# Nipashe

Jumatatu Machi 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580527

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**Askofu**
Niwemugizi ataka viongozi kuenzi mema ya JPM

UKURASA 4



**BAKWATA**
wamkumbuka kuthamini viongozi wa dini

UKURASA 4



**Neymar atabiriwa kucheza tena na Lionel Messi**

UKURASA 20

# Marais 10 Afrika kumzika JPM



• **Mamia** washindwa kuaga Dar, maziko kitaifa Dodoma leo... *Endelea Ukurasa 2, 3*



Askari Mgambo wakimsaidia mmoja wa waombolezaji aliyepoteza fahamu baada ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, wakati wa kutoa heshima za mwisho katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play
App Store


# Chato yafurika wageni, wengi wakosa pa kulala

UKURASA 3


**MICHEZO** WAACHIA 'KALALE PEMA PEPONI MAGUFULI' UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



# Marais 10 Afrika kushiriki maziko

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIONGOZI wa kimataifa kutoka nchi mbalimbali wakiwamo marais 10, leo watashiriki maziko ya kitaifa na kutoa heshima ya mwisho kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Jamhuri, jijini hapa.

Marais hao ni pamoja na wa Kenya, Uhuru Kenyatta, wa Msumbiji, Filipe Nyusi, wa Malawi, Lazarus Chakwera, wa Comoro, Azali Athuman na wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa.

Wengine ni Rais wa Zambia, Edgar Lungu, wa Botswana, Mokgweetsi Masisi wa Afrika ya Kusini, Cyril Ramaphosa, wa Namibia, Dk. Hage Geingob na wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Felix Tshisekedi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alisema viongozi wengine wanaowakilisha marais wao ni Waziri Mkuu wa Rwanda, Makamu wa Rais Burundi na Waziri wa Mambo ya Nje wa Angola.

"Kutakuwa na mabalozi, wakuu na wawakilishi jumuiya za kimataifa na asasi za kikanda ikiwamo Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Mataifa ofisi ya Tanzania ambao ni zaidi ya 50 watashiriki, taratibu za uthibitisho bado zinaendelea," alisema.

Alisema leo ni maziko ya kitaifa na viongozi watatoa heshima ya mwisho na shughuli zitaanza saa tatu asubuhi katika uwanja huo.

"Mwili ukitoka Ikulu Chamwino utaanzia bungeni ili wabunge wapate fursa ya kumuaga kiongozi wetu na baadaye mwili utakuja hapa uwanjani, baada ya viongozi kuaga, wataanza kuaga wananchi na tutajitahidi waage hadi usiku kwasababu ni siku moja tu," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliwaomba wananchi kuanza kuingia uwanjani kuanzia saa 12:00 asubuhi ili wapate fursa ya kuaga mwili.

Alisema mwili huo utatoka Ikulu ya Chamwino kwa kupitia barabara mpya ya Mfugale, Buigiri, Morena, Bunge, round about ya Mkuu wa Mkoa, Barabara ya Nyerere na kufika Uwanja wa Jamhuri.

"Rais Samia Suluhu Hassan, ataongoza waombolezaji wote katika zoezi la kuaga na kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa mpendwa wetu na zoezi litaendelea hadi wananchi watakapomalizika na baadaye mwili utapelekwa Hospitali ya Benjamin Mkapa kuhifadhiwa na asubuhi utasafirishwa kwenda Zanzibar," alisema.

Alisema pia kutakuwapo na wakuu wa mikoa wote, viongozi wa vyama vya siasa, wakiongozwa na CCM wa dini na makundi mbalimbali.

"Miongoni mwa mambo muhimu yatakayofanyika katika Uwanja wa Jamhuri, ni pamoja na kuwa na gwaride la mazishi kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania, dua na sala kutoka kwa viongozi wetu wa dini, salamu mbalimbali za maombolezo kutoka kwa viongozi mbalimbali, kuaga na kutoa heshima za mwisho," alisema.

Alisema Machi 23, saa 12:00 asubuhi, mwili wa Hayati Magufuli utaondoka Hospitali ya Benjamin Mkapa kwenda Uwanja wa Ndege wa Dodoma kupitia barabara za UDOM, Chimwaga, Morena, Bunge round about ya Mkuu wa Mkoa, Chako ni Chako hadi Airport na kuelekea Zanzibar.

**BUNGE KUMUAGA**

Mwili kabla ya kupelekwa Uwanja wa Jamhuri utaanzia kuagwa na bungeni saa mbili asubuhi ili kutoa fursa kwa wabunge.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, akisaini kitabu cha maombolezo ya Dk. John Magufuli alipowasili ofisi ya CCM Mtaa wa Lumumba kuhudhuria kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, kilichofanyika juzi. **PICHA: IKULU**

# Aagwa kifalme Dar, mamia wakosa fursa

**Na Elizabeth Zaya**

NI kama mfalme! Ndivyo ilivyoonekana katika Uwanja wa Uhuru katika siku mbili ambazo wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, walipewa nafasi ya kumuaga mpendwa wao Hayati Rais Dk. John Magufuli, baada ya uwanja huo kufurika na kulazimika kufungwa kwa milango mikuu ya kuingilia.

Utaratibu wa kuaga mwili huo, ulibadilishwa kwa wananchi kulazimika kupanga mistari minne na kuaga kwa kupita nje ya kibanda maalumu kilichowekwa jeneza la mwili wa Hayati Dk. Magufuli, badala ya ndani kama ilivyokuwa awali.

Hali hiyo ilitokana na uwanja kuzidiwa na umati wa watu waliokuwa na hamu ya kumuaga aliyekuwa rais wao na milango mikuu ya kuingia ndani ya uwanja huo kufungwa huku waliokuwa nje kuzuiwa kuingia mpaka waliokuwa ndani wamalize kuaga.

Barabara mbalimbali ambazo mwili wa Hayati Rais Dk. John Magufuli, ulipitishwa jana na juzi, wananchi walioijitokeza kumuaga walitandika khanga, fulana barabarani na kurusha maua kwenye gari lililobeba mwili wake, huku wengine wakiangua kilio na kujaribu kulishika gari hilo.

Mwili wa Hayati Rais Dk. Magufuli jana ulipelekwa katika Uwanja wa Uhuru, ikiwa ni siku ya pili ya kumuaga kiongozi wao aliyewaongoza kwa miaka mitano na miezi minne, kabla ya kupelekwa jijini Dodoma, ambako wananchi wa huko pia watapata fursa ya kumuaga na pia utapelekwa visiwani Zanzibar, jijini Mwanza, mjini Geita na hatimaye maziko Machi 26, kijijini kwake Chato.

Kwa siku mbili wananchi wa Dar es Salaam, walijitokeza kwa maelfu huku wengine wakishindwa kujizuia kulia na kuanguka baada ya kuona mwili wake ukiwa umelala kwenye jeneza.

Katika barabara ambazo mwili huo ulipitishwa, baadhi ya watu walitandika khanga na nguo zao, wengine wakizipeperusha kama bendera na kurusha maua na matawi ya miti ikiwa ni ishara ya kuonyesha upendo kwa kiongozi wao.

Baadhi ya wananchi walionekana kupiga magoti na saluti kukubali kile alichowafanyia wakati wa uhai wake.

Mabango yenye ujumbe yalibebwa na wakazi wa Jiji la Dar es Salaam huku baadhi yakiandikwa,

***'Umeondoka Chuma cha Afrika', 'Umetuacha mtetezi wa wanyonge'.***

Miongoni mwa maeneo ambayo mwili ulipitishwa wakati wa kwenda kulazwa katika Hospitali ya Jeshi Lugalo juzi usiku baada ya kuhitimisha siku ya kwanza ya kuagwa ni daraja la juu la Dk. Kijazi, Ubungo, ambalo ujenzi wake ulisimamiwa na Hayati Dk. Magufuli. Kundi kubwa la vijana lilijitokeza na kusindikiza msafara huo kwa kukimbia mchakamchaka na kuimba nyimbo za kumuaga.

Siku ya kwanza mwili wa Hayati Dk. Magufuli ulipitishwa katika Barabara ya Uhuru, Ali Hassan Mwinyi, Morocco na Chang`ombe.

Siku ya pili, ulipitishwa Mwenge, Barabara ya Sam Nujoma, kuelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hadi Ubungo, Barabara ya Morogoro kupitia Manzese na Kawawa ambako wananchi walifurika wakiimba na kulia na kutandika nguo na matawi barabarani.

Waendesha bodaboda waliufuata msafara uliokuwa umebeba mwili wa shujaa huyo wakipiga ving`ora huku wakiimba nyimbo na kuupigia saluti jeneza lililobeba mwili wa hayati Dk. Magufuli katika gari maalum la kijeshi lililokuwa likiongozwa na Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Katika baadhi ya maeneo wananchi walishindwa kujizuia na kulazimika kulisogelea gari hilo kwa kutaka kuligusa jambo lililowalazimu Askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) kuwazuia na kulisogelea gari hilo.

Maeneo ya Karume, Ilala Boma, Mwenge, Mansese, Magomeni ambako kuna vituo na idadi kubwa ya wafanyabiashara ndogo (Machinga), yalifurika kwa waombolezaji.

Jana msafara uliobeba mwili wa Hayati Dk. Magufuli, ulianza safari saa 1.40 asubuhi kutoka Hospitali ya Jeshi Lugalo na kufika saa 8:28 Uwanja wa Uhuru ambao ulikuwa umefurika watu majukwaa yote huku wananchi wengine wakilazimika kukaa nje.

Wanawake kwa wanaume, watoto kwa vijana pamoja na wazee baadhi yao baada ya kuaga walizimia na vikosi vya usalama vilivyokuwa vimejipanga katika eneo hilo pamoja na kikosi cha msalaba mwekundu kulazimika kuwasaidia kwa kutoa huduma ya kwanza.

**UHURU HAPATOSHI**

Jana Uwanja wa Uhuru ulionekana kuzidiwa baada ya majukwaa yote kufurika na watu wengine kulazimika kubaki nje.

Viongozi waliokuwa wakisimamia kazi ya kuaga kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama walilazimika kufunga mageti ili walio nje wasiingie mpaka waliokuwa ndani wamalizike.

Hata hivyo, baadhi ya waombolezaji hawakutii utaratibu huo na kuamua kupanda juu ya uzio kurukia ndani na wengine kupenya kwenye sehemu za matundu bila kujali askari waliokuwa wakiwazuia.

Waongozaji na wasimamizi wa kazi hiyo ya kuaga, akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, walilazimika kuwatuliza waombolezaji ambao walikuwa wakisukumana kuingia ndani kwa kuwasisitiza kuwa hakuna mwananchi atakayeondoka bila kutoa heshima za mwisho kwa mpendwa wao.

Baadhi ya wananchi walisema walifika uwanjani hapo kabla ya saa 12 asubuhi kwa ajili ya kuwahi kujipanga ili wapate nafasi ya kuaga mwili wa Hayati Dk. Magufuli.

**GARI ZA KUBEBEA WAGONJWA**

Ndani na nje ya uwanja Kikosi cha Msalaba Mwekundu na vikosi vya ulinzi na usalama vilikuwa na kazi ya ziada ya kuwasaidia na kuwabeba katika machela watu waliokuwa wakizimia.

Gari za kubebea wagonjwa zilikiwa zikipishana uwanjani kubeba watu waliokuwa wakizimia.

Badala ya kazi hiyo ya kutoa heshima za mwisho kumalizika saa tisa alasiri, ilibidi uongezwe hadi saa moja jioni ili kutoa nafasi kwa wote waliokuwa wamejitokeza uwanjani hapo kuaga.



# Chato yafurika wageni, wengi wakosa pa kulala

**Na Richard Makore,** CHATO

IDADI ya watu waliofika mjini Chato mkoani Geita kwa ajili ya kuhudhuria maziko ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, imesababisha huduma muhimu zikiwamo nyumba za kulala wageni kujaa, huku baadhi wenye nyumba hizo wakihamisha wateja kwa madai kwamba vyumba vimelipiwa na watu wasiojulikana.

Baadhi ya wageni wamelalamikia wenye nyumba za kulala wageni kwa kuwaambia waondoke kwenye vyumba kwa madai kwamba vimelipiwa.

Mmoja wa wateja waliokutwa na mkasa wa kutakiwa kuhama nyumba ya wageni, Desteria George, alisema alifika mjini Chato akitokea mkoani Iringa kwa ajili ya kuaga mwili wa Hayati Magufuli, na kwamba ameambiwa aondoke kwa madai kwamba chumba chake kimechukuliwa.

Aiidha, baadhi ya wafanyabiashara wa migahawa wamesema tangu kifo cha Hayati Dk. John Magufuli kutangazwa, wamekuwa na wateja wengi kuliko huko nyuma.

Walisema kutokana na wateja kuongezeka na wao wameongeza wafanyakazi katika migahawa hiyo.

Mmoja wa wahudumu katika mgahawa wa Glory uliopo mjini Chato, Paulina Mabela, alisema kwa sasa wanapata wateja wengi kuliko siku za nyuma, na kwamba kutokana na wateja kuongezeka na wao wameongeza kipimo cha vyakula wanavyopika kwa siku.

Kwa upande wa waendesha bodaboda nao wameongezeka baada ya wilaya za jirani kuingia mjini Chato kwa ajili ya kutafuta riziki.

Baadhi ya bodaboda wamesema wameshangaa kuona watu ambao hawajui wakiwa katika vituo mbalimbali vya bodaboda, na kwamba baada ya kuwauliza walisema wanatoka wilaya jirani na Chato.

Baadhi ya shughuli zimesimama ikiwamo kufungwa maduka, huku baadhi ya watu wakionekana kukaa katika makundi makundi wakijadili kifo cha Hayati Magufuli.

# Wamachinga wasimamisha biashara JPM akiagwa leo

**Paul Mabeja na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKATI maziko ya kitaifa ya Dk. John Magufuli yakifanyika leo, wamachinga mkoani Dodoma wamesema hawatafanya biashara zao kwa siku moja kwa ajili ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais John Magufuli.

Mwenyekiti wa umoja wa Machinga mkoani Dodoma, Bruno Mponzi, alisema lengo ni kuhakikisha wanashiriki kikamilifu kwa pamoja kuaga mwili huo kwa kuwa alikuwa mtetezi wao katika kipindi chote cha uhai wake.

Mponzi alisema kuwa masoko yote ambayo kuna machinga wanaofanya biashara zao siku hiyo itabidi wasifanye biashara kwenye maeneo yao ili kushiriki kikamilifu na waweze kuungana kwa pamoja kuaga mtetezi wao.

Alisisitiza wataendelea kumuenzi Rais Magufuli kutokana na mchango mkubwa aliouonyesha kwa machinga nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amesema kuwa maandalizi yote muhimu kwa ajili ya shughuli za kuaga mwili wa hayati Rais Dk. John Magufuli yamekamilika huku akiwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kutoa heshima zao za mwisho. Dk. Mahenge aliyasema hayo jana jijini Dodoma, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi hayo.

"Mwili wa mpendwa wetu Dk. John Pombe Joseph Magufuli, utawasili katika uwanja wa ndege wa Dodoma Jumapili tarehe 21 Machi, 2021 (jana) majira ya saa 10:00 jioni," alisema Dk. Mahenge.

Baada ya kuwasili mwili huo utaelekea Ikulu ya Chamwino kwa kupitia Barabara za Chako ni Chako, Barabara ya Nyerere, round about ya Mkuu wa Mkoa, Bunge, Morena, Bwigiri- Chamwino-Ikulu, wananchi wote wa maeneo haya wanaombwa kujipanga kwenye barabara hizo kutoka heshima zao.

"Tarehe 22 Machi, 2021, Saa 12:00 asubuhi, mwili wa mpendwa wetu Hayati Rais Dk. John Pombe Joseph Magufuli utatoka Ikulu kuja Uwanja wa Jamhuri kwa kupitia barabara mpya ya Mfugale, Bwigiri, Morena, Bunge, Round About ya Mkuu wa Mkoa, Barabara ya Nyerere, Uwanja wa Jamhuri, wananchi wa maeneo hayo mnaombwa kujitokeza kwa wingi," alisema.

Leo ni siku ya kuaga mwili na kutoa heshima za mwisho kwa Hayati Rais Dk. John Magufuli katika Mkoa wa Dodoma.

"Siku hii pia itakuwa ni ya mapumziko kama alivyoelekeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan," alisema.

Alisema shughuli ya kuaga mwili na kutoa heshima za mwisho itafanyikia katika Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 12:00 -3:00 asubuhi.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ataongoza waombolezaji wote katika zoezi la kuaga na kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa mpendwa wetu hadi wananchi watakapomalizika," alisema.

Pia alisema viongozi wengine watakaoshiriki ni pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, viongozi wengine wa kitaifa wa serikali, Bunge na Mahakama, viongozi wa Jumuiya na Taasisi za Kimataifa, Mabalozi na Viongozi kutoka nchi mbalimbali.

Alisema pia wakuu wa mikoa wote, viongozi wa vyama vya siasa watatoa heshima zao wakiongozwa na viongozi wa CCM, viongozi wa dini na makundi mbalimbali.

"Miongoni mwa mambo muhimu yatakayofanyika katika Uwanja wa Jamhuri ni pamoja na kuwa na gwaride la mazishi kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania, dua na sala kutoka kwa viongozi wetu wa dini, salamu mbalimbali za maombolezo kutoka kwa viongozi mbalimbali, kuaga na kutoa heshima za mwisho," alisema Dk. Mahenge.

*Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afisa wa Kupambana na Fedha Haramu*

esaamlg

## RAMBIRAMBI



**Mh. Dkt John Pombe Joseph Magufuli**
**1959 – 2021**

Baraza la Mawaziri, Kikosi Kazi cha Maofisa Waandamizi na Watanyakazi wa Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini Mwa Afrika wa Kupambana na Fedha Haramu wamepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli.

Tunatoa Salaam za pole kwa Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na Serikali yote, Mama Janet Magufuli na Familia yako na Watanzania wote kwa ujumla.

***Roho ya Marehemu ipate Rehema kwa Mungu na ipumzike kwa Amani.***

**Eastern and Southern Africa**
**Anti – Money Laundering Group**
**ESAAMLG Secretariat**
**Website: www.esaamlg.org**

WOMEN FUND TANZANIA-TRUST
Empowering Local Women Heroes



@womenfund_tz
@wft.tz

**Hayati Dkt John Pombe Magufuli**
**Raisi wa Awamu ya Tano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania**

Taasisi ya Women Fund Tanzania Trust imepokea kwa masikitiko na mshtuko mkubwa taarifa ya kifo cha Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Raisi wa Awamu ya Tano ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021. Tunatoa Pole za dhati kwa Mhe. Raisi Samia Suluhu Hassan, Serikali, Watanzania, Mama Janeth Magufuli, na familia yote.

Hili ni pigo kubwa kwa taifa letu na kipindi kigumu kwa wote.
Ni matumaini yetu kuwa tutaenzi michango yake katika kusimamia misingi ikiwa na nia ya kufikisha rasilimali ya taifa kwa wananchi walio wengi zaidi.



# Niwemugizi awataka viongozi kuenzi aliyoanzisha Magufuli

**Na Richard Makore,** CHATO

ASKOFU wa Jimbo la Katoliki la Rulenge Ngara, mkoani Kagera, Severine Niwemugizi, amewashauri viongozi waliobaki nchini kutenda mema na kuyaenzi mambo aliyoyaanzisha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Alitoa ushauri huo jana, katika ibada iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Jimbo la Rulenge Ngara lililopo mjini Chato ambalo marehemu alibatizwa.

Askofu Niwemugizi aliwaomba viongozi hao kutenda mema na kuonyesha mshikamano katika kipindi hiki cha msiba wa taifa.

Aliongeza kuwa Hayati Dk. Magufuli alikuwa muuni wa kweli na kila alipokuwa nyumbani kwao Chato, alikuwa akisali hapo.

Katika hatua nyingine, Askofu Niwemugizi alisema mwili wa Hayati Dk. Magufuli unatarajiwa kusaliwa katika kanisa hili mjini Chato Alhamisi wiki hii kisha kupelekwa katika uwanja maalum ulioandaliwa kwa ajili wananchi kuuaga.

Alisema Hayati Magufuli alikuwa muumini katika kanisa hilo na kwamba kanisa hilo pamoja na waumini wake watamkumbuka kwa mema aliyofanya akiwa duniani.

Aliwaomba waumini wa kanisa hilo na wananchi wengine kujitokeza katika misa hiyo.

Kwa upande wake, Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Jimbo la Bihamulo lililopo mjini Chato, Samson Zakaris, alisema hayati Magufuli alifanya mambo mengi na mema kabla ya kifo chake.

Aliwaomba waumini wake kumuenzi Hayati Magufuli kwa kufanya kazi na kushikamana katika kipindi hiki kigumu cha msiba.

Alisema Hayati Magufuli amemaliza kazi yake duniani na kwamba Watanzania wamwombee kwa Mungu.

Hayati Magufuli aliyefariki Machi 17, mwaka huu, jijini Dar es Salaam anatarajiwa kuzikwa Ijumaa nyumbani kwake Chato.

# BAKWATA: Aliwathamini viongozi wa dini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Baraza Waislam Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma, imesema itamkumbuka Hayati Rais John Magufuli, kwa kuwapa kipaumbele viongozi wa dini katika kipindi chote cha utawala wake.

Hayo yalibainisha jana na Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kifo cha Rais Magufuli.

Bashiru, alisema katika kipindi cha utawala wa Rais Magufuli, viongozi wa dini walipewa kipaumbele, hali iliyosababisha kuheshimika hata walipokuwa wakiingia katika ofisi za umma.

Alisema katika matukio mbalimbali Rais Magufuli alihakikisha kuwa viongozi wa dini wanapewa kipaumbele ikiwamo kwenye uzinduzi wa miradi mikubwa ya kimkakati.

"Mimi binafsi siwezi kumsahau Rais Magufuli, ametufanyia mengi ukiondoa ile miradi ya kijamii lakini pia kwenye dini alitujengea msikiti mkubwa pale Chamwino na mimi siku ile nilimwakilisha Shekhe wa Mkoa kutoa salamu za BAKWATA," alisema Bashiru.

Aidha, alisema pamoja na kujenga msikiti, pia Rais Magufuli alishiriki katika ujenzi wa makanisa mbalimbali nchini.

"Kutokana na kifo hiki cha ghafla cha mpendwa wetu, nitoe wito kwa Watanzania kuendelea kushikamana kwa pamoja na kuwa waaminifu na kuendeleza umoja wetu," alisisitiza Bashiru.

Pia alisema miradi mikubwa ya kimkakati ambayo Rais Magufuli aliyoiacha, viongozi waliobaki wanatakiwa kuitekeleza ili kuwa sehemu ya kumuenzi.

"Kuna miradi ambayo Rais Magufuli, alikuwa amepanga kuitekeleza katika kipindi chake kabla ya kufikwa na umauti, viongozi waliobaki wasirudi nyuma wahakikishe kuwa inakamilika, hapa Dodoma alipanga kujenga uwanja wa ndege pamoja na uwanja wa mpira," alisema.

# Makamu wa Rais Marekani ampongeza Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, amempongeza rais wa sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Hassan Suluhu, kwa kushika nafasi ya juu ya uongozi wa nchi.

Katika ukurasa wake wa Tweeter, Kamala aliandika; "Natuma pongezi zangu kwa Samia Hassan Suluhu baada ya kuapa kuwa rais mpya wa Tanzania, mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo."

"Marekani iko tayari kufanyakazi na wewe katika kuimarisha uhusiano baina ya nchi zetu."

Pia katika ukurasa wa Ubalozi wa Marekani nchini ambao waliambatanisha salamu za Makamu huyo wa Rais, waliandika "Makamu wa Rais Marekani ametuma ujumbe wa hongera kwa Rais Samia Hassan Suluhu."

Wachangiaji wengine katika ukurasa huo, Morgaine Pendragona aliandika "Kuongoza; wanawake wanakwenda kuongoza dunia, hii ndiyo tofauti ya mfumo dume na ushirika wa thamani."

Ujumbe mwingine; "Historia imeandikwa Afrika MasharIki, Samia Hassan Suluhu kuwa Rais wa Tanzania kama Rais mwanamke wa kwanza kuwa mkuu wa nchi kwa sasa Afrika."

Naye Global Peace aliandika; "Binafsi nafikiri duniani itakuwa mahala pazuri kama tutakuwa na wanawake viongozi wengi wanaoendesha nchi, hasa katika maendeleo ya nchi, kiuhalisia kila mahali kuna rekodi za uongozi wa wanaume ulio wa rushwa na udikteta."

Fernando Ebora, aliandika; "Umeongoza vizuri sana tunahitaji wanawake viongozi wenye moyo safi, siyo dikteta wanaoiba fedha za nchi zetu, tunatumaini nasi (USA) tutachagua viongozi wanawake kwenye uchaguzi ujao."

Katika ukurasa huo, Doroth Musya aliandika; "Tunahitaji wanawake wengi kwenye madaraka ya kisiasa tutabadili dunia, mahali nilipo tumchague Seneta mwanamke, afadhali mwanamke, tuwakuze viongozi wanawake."

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), aliandika "Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres anatoa salamu za pongezi kwa Mh. Samia Hassan Suluhu baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Tanzania, mwanamke wa kwanza kuwa mkuu wa nchi."

Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Amina Mohamed, katika ukurasa wake aliandika "Naungana na Katibu Mkuu kuwasilisha salamu za pongezi kwa Mh Samia Hassan Suluhu Rais wa Tanzania. Ni wakati wa historia ya uongozi wa wanawake Afrika na duniani. "

CONSORTIUM FOR STREET CHILDREN

## Taarifa Kwa Umma

Tafadhali jihadhari na utapeli unaofanywa na kikundi cha watu wanaotumia jina la Shirika la Consortium for Street Children - CSC ili kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu. Utapeli huu unafanyika jijini Mwanza na pengine katika maeneo mengine nchini Tanzania.

Jina na nembo ya shirika la Consortium for Street Children vinatumika kwa ajili ya kudanganya watu kutoa fedha. Consortium for Street Children ni shirika lisilo la kiserikali lenye usajili nchini Uingereza na linajishughulisha na watoto wa mtaani. Shirika hili halichangishi fedha nchini Tanzania na halihusiani na watu wanaosambaza fomu za kuchangisha fedha hizo kwa namna yoyote. Kujaza fomu wanazosambaza hakutapelekea kufaidika na jambo lolote lile wanaloliahidi. Kama umefuatwa na watu kwa ajili ya kujaza fomu au kuchangia fedha, au una taarifa zozote kuhusiana na utapeli huu, tafadhili toa taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nawe.

**TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI**

**Ana Mwaitege** mkazi wa viwanja vya Mwadui Manispaa ya Shinyanga.

Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 322 BXB SANLG** ina rangi nyekundu Injini namba **18905810.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Ana Mwaitege kwa simu namba **0757919892.** **Rb namba/ShyRb/ 2021, Control namba 9910820807323.**

**TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI**

**Julius Daniel Maguja** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari yenye namba za usajili **T. 940 CJD** Toyota Ipsum Rangi nyekundu injini namba **2AZ0600534.** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Julius Daniel Maguja kwa simu namba **0759032275. RB namba/ShyRB/2021/** control namba **9910820809802.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU DAR ES SALAAM**

**KESI YA "MADAI" NA. 5 YA MWAKA 2021**

**SAMASON AGINGA……………..MDAI**

**DHIDI YA**

**RASHID SHABANI MANGARA……………..MDAIWA**

**KWA: RASHID SHABANI MANGARA POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 23/03/2021 saa 07:00 mchana.

ANGALIA: Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 18 Mwezi wa Machi, 2021.

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU - DAR ES SALAAM

## TANGAZO


# tigo pesa — Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Ada kwa mteja (Tsh) | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM |
| 100 | 999 | 15 | 15 | N/A |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 50 | 300 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 50 | 400 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 100 | 600 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 100 | 650 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 200 | 950 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 200 | 1,000 |
| 10,000 | 19,999 | 360 | 550 | 1,450 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 600 | 1,850 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 680 | 1,850 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 750 | 2,350 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 1,250 | 2,700 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,600 | 3,650 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,900 | 5,300 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 2,300 | 6,500 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 2,500 | 7,000 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 3,200 | 7,500 |
| 600,000 | 799,999 | 3,300 | 4,300 | 8,000 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 4,300 | 8,000 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 6,000 | 8,000 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 6,000 | 8,000 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 6,000 | 10,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma Pesa kwa mteja ambaye amesajiliwa ila hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa Pesa kwa mteja ambaye amesajiliwa ila hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika** kwa Ada za huduma nyingine tembelea tovuti; **https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:**

**KUMBUKA:**

1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN) kwa usalama. Usimpe wala kumtajia mtu yeyote namba yako ya siri; iwe wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa Wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Kutuma muamala wa zaidi ya TSh 5,000,000 ni kwa wafanyabiashara waliosajiliwa pekee.
8. Tigo itakupigia kwa 0713800800 au 0713123103 Tu.
9. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwa barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
10. Unaweza kupokea pesa kutoka zaidi ya Nchi 150 duniani

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#**
chagua **6 (Jihudumie)**
kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!




**Fanya malipo ya Serikali**

TRA

SUMATRA

TANESCO LUKU

Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia June 2020

tigo

www.tigo.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanamichezo nchini wamuenzi Magufuli kwa ushindi, makombe

**MACHI** 17, mwaka huu, itabaki kuwa siku ya kukumbukwa nchini baada ya Watanzania kumpoteza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia majira saa 12 jioni kwa maradhi ya moyo katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam.

Kwa sasa Watanzania wanaendelea na maombolezo kwa siku 21 kuanzia Machi 17, wakati huu maziko ya Hayati Magufuli yakitarajiwa kufanyika Ijumaa Machi 26, mwaka huu, nyumbani kwake, Chato mkoani Geita.

Hakika ni majonzi makubwa kwa Watanzania kutokana na juhudi kubwa ambazo Magufuli alianza kuzionyesha katika kuhakikisha sekta ya michezo nchini inakua kwa kasi na kuitoa Tanzania katika 'kichwa cha mwendawazimu' pindi linapokuja suala la michezo kimataifa.

Kwa hakika Magufuli ametangulia mbele ya haki, hatunaye tena katika dunia hii, lakini kauli zake zinaendelea kuishi hususan ile aliyoitoa Mei 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa (sasa kwa Benjamin Mkapa), wakati akiikabidhi Simba Kombe la Ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa msimu wa 2017/18.

Magufuli alisema yeye kama kiongozi atafurahi sana siku moja akiitwa kukabidhi Kombe la Afrika litakalochukuliwa na timu yoyote hapa nchini, hivyo akaiomba Simba ikawe klabu ya kwanza kuleta Kombe la Afrika hapa Tanzania.

Tunatambua Dk. Magufuli alitumia nafasi hiyo kufikisha ujumbe huo si kwa Simba pekee ama klabu za soka pekee, bali kwa timu zote zinazopata dhamana ya kuipeperusha bendera ya Tanzania katika michezo mbalimbali kimataifa.

Hivyo, huu ni wakati kwa klabu, mchezaji mmoja mmoja ama timu yoyote inayopata nafasi kwenda kuiwakilisha Tanzania kwenye michezo ya kimataifa, kuibeba kauli hiyo ya Magufuli na kutambua kuwa kiongozi wao waliyempenda kutokana na juhudi zake kubwa kulitumikia taifa hili, alitamani kuona nchi yake ikileta medali na makombe kupitia michezo mbalimbali.

Katika kuhakikisha hilo linatimia, Magufuli alianza kuonyesha jitihada kubwa kwenye sekta ya michezo ikiwa ni pamoja na kuahidi kujenga uwanja mkubwa wa soka jijini Dodoma akishirikiana na Serikali ya Morocco, lakini tumeshuhudia kwa mara ya kwanza serikali yake ikitangaza kubeba bajeti zote za kuhudumia timu za taifa jambo ambalo halikuwahi kufanyika hapo kabla. Hivyo, wakati huu ambao timu ya soka ya Taifa, Taifa Stars ikijiandaa kucheza mechi mbili za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), dhidi ya Equatoria Guinea na Libya, inapaswa kutembea na kauli hiyo ya Magufuli kwa kulenga ushindi ili kufuzu fainali hizo kwa mara ya tatu na ya pili mfululizo na hatimaye kwenda kupigania taji hilo.

Lakini kwa upande wa klabu, Simba na Namungo zinaiwakilisha nchini kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika mwaka huu, hivyo hazina budi kutembea na kauli hiyo huku zikiitendea haki ili kumaliza kiu ya Magufuli aliyokuwa nayo ya kuona siku moja timu kutoka Tanzania zinatwaa ubingwa wa Afrika.

Tunaamini hilo linawezekana kama kila mchezaji katika michezo mbalimbali, ataamua kujitoa kuhakikisha Tanzania inakuwa moja kati ya nchi ya kuogopwa linapokuja suala la michezo kwa timu za hapa nchini.

Katika hilo, Nipashe tunatamani kuona kila mchezaji, klabu ama timu yoyote inayoiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kuwa na kiu ya kuwa ya kwanza kutekeleza kauli hiyo ya Magufuli kwa vitendo kwa kubeba ubingwa wa kwenye michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba hakikisheni mnalipa deni hili la Hayati Magufuli kimataifa

Na Adam Fungamwango

**"MIMI** kama kiongozi wenu nitafurahi sana siku moja mkiniita hapa kuja kukabidhi Kombe la Afrika litakalochukuliwa na timu yoyote katika nchi yetu. Kwa hiyo niwaombe Simba mkawe wa kwanza basi kuleta Kombe la Afrika hapa Tanzania." Yalikuwa ni maneno ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu.

Kauli hiyo aliitoa Mei 19, 2018 kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Mkapa), akiikabidhi Kombe la Ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa Simba msimu wa 2017/18 uliohitimishwa kwa mechi dhidi ya Kagera Sugar.

Ilikuwa ni moja ya mechi ya kukamilisha ratiba, lakini Simba ilifungwa bao 1-0. ilikuwa ni bao la dakika ya 84 lililofungwa na Edward Christopha. Matokeo hayo yalionekana kumkasirisha Magufuli.

Na si matokeo tu, hata aina ya uchezaji. Akawapasha kuwa hakuridhika na uchezaji huo na kuwaambia kama watakwenda kucheza Ligi ya Mabingwa basi hawatofua dafu, na kuwashauri kuboresha kikosi chao.

Baada ya hapo klabu ya Simba ilionekana kutembelea kauli ya Magufuli kwa kubadilika, ikitengeneza kikosi bora taratibu kila msimu, ikisajili wachezaji wenye viwango vya hali ya juu, kiasi cha sasa kuwa ndiyo timu yenye kikosi bora nchini Tanzania pengine hata Afrika Mashariki na Kati.

Maneno hayo yaliifanya Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2018.

Hadi anafariki dunia, tayari kwa mara nyingine tena, Simba inakaribia kutinga tena hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na safari hii ikiongoza Kundi A, ikiwa na pointi 10, juu ya Mabingwa Watetezi Afrika, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan.

Kwa sasa inahitaji pointi moja tu ili iweze kufuzu na kuweka tena rekodi ya mwaka 2018. Magufuli alisema angefurahi timu yoyote ile nchini itwae ubingwa wa Afrika. Lakini akaiomba Simba iwe ya kwanza kufanya hivyo. Hakusema kwa bahati mbaya.

Ni kwamba bado historia ya soka nchini inaibeba Simba kuwa ndiyo timu yenye mafanikio zaidi linapokuja suala la mechi za kimataifa. Imeshawahi kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 1974 na finali ya Kombe la CAF, sasa Shirikisho, mwaka 1993. Kwa sababu hiyo aliona inaweza kufika mbali.

Wachambuzi wa masuala ya soka Afrika wanasema mara nyingi timu zinazotwaa Kombe la Afrika ni zile ambazo zinaishi kwenye hatua za ngazi ya makundi. Yaani hazikosekani. Halafu zinaishia robo, nusu au fainali. Kama ukiona timu huwa haifiki sehemu hiyo, basi haina sifa za ubingwa huo.

Ni ngumu sana timu ambayo inashiriki mara chache na inaanza hatua za awali moja kwa moja iende kutwaa kombe hilo. Ni mpaka iwe na sifa hizo tu. Ndiyo maana angalau aliiona Simba ina sifa hizo.

Kwa sasa ina sifa hizo. Hata kama haikuchukua ubingwa msimu huu, lakini tayari imekuwa timu ambayo hata ikitokea miaka michache ijayo ikatwaa kombe hilo hakuna shabiki yeyote Afrika atashtuka. Imeshaanza kujipambanua kuwa moja ya timu kubwa, ngumu na tishio.

Lakini kabla hajaitwa kukabidhi Kombe la Afrika, Magufuli amefariki. Amefariki akiwa hajatimiza kile alichoona kinawezekana baada ya miaka kadhaa. Ni wajibu sasa wa viongozi wa Simba, wanachama, mashabiki na wachezaji kuchukua kifo hicho kama deni ambalo wameachiwa.

Na hii inaweza kuanzia kwenye mechi dhidi ya AS vita. Awali alivyosema Simba kuchukua Kombe la Afrika ilionekana kama anaongea mzaha au kitu kisichowezekana. Lakini kwa sasa kwa Simba ni kitu ambacho kipo kwenye mikono yao. Hata kama si msimu huu, basi haipo mbali na hilo. Na hata mashabiki wa timu hiyo wameanza kuamini kuwa wanaweza.

Kifo cha Magufuli kiwafanye Simba kupambana kweli ili kuweza kutwaa kombe hilo. Na ikilitwaa basi mtu wa kwanza kukumbukwa itakuwa yeye. Kwa sababu ndiye aliyewapa chachu. Aliyewaambiwa wanaweza kuchukua Kombe la Afrika kama wakiamua kubadilika.

Kubadilika ni uwekezaji, uongozi kuwa na mipango madhubuti, kupata wachezaji wenye viwango vya hali ya juu na umoja. Vyote hivyo kwa sasa vipo, hivyo natarajia wachezaji, benchi la ufundi na uongozi wa klabu hiyo, wakiishi na kauli hiyo ili kuikamilisha kama walivyoagizwa Dk. Magufuli ambaye hatunaye tena kwa sasa.

Tpb Bank
Grow with us

# BURIANI





Kwa huzuni na masikitiko makubwa tumepokea habari kuhusu kifo cha
Rais wa Awamu ya Tano wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Mhe. Dr John Pombe Magufuli.**

Rais Magufuli alikuwa mzalendo halisi aliyeiongoza nchi katika kipindi kigumu kwa busara na maono makubwa.

Katika kipindi hiki cha maumivu makubwa, sisi Benki ya TPB, tunapenda kutoa rambirambi zetu kwa serikali na kwa taifa kwa ujumla.

Fikra na sala zetu pia ziende kwa familia ya marehemu Rais Magufuli.

Tunaiombea kwa Mwenyezi Mungu kuwapa nguvu na subira kutokana na kuondokewa kwa mwanafamilia."



**MWENYEZI MUNGU AIPUMZISHE
ROHO YAKE KWA AMANI.**

www.tpbbank.co.tz || info@tpbbank.co.tz,
marketing@tpbbank.co.tz || facebook/tpbbank || 0787 669977



# Mpanju: Samia ana nafasi ya kufanya makubwa

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ana nafasi ya kufanya makubwa zaidi ya mtangulizi wake hayati, Dk. John Magufuli.

Alisema Samia ana nafasi ya kufanya makubwa kwa sababu maendeleo na miradi yote iliyokuwa ikitekelezwa na hayati Dk. Magufuli alikuwa anafahamu na alikuwa akisaidia kuifanikisha kulingana na nafasi yake.

Kinachotakiwa, alisema ni kuhakikisha anapewa ushirikiano.

"Mama Samia ana nafasi ya kufanya vizuri zaidi kuliko hata mtangulizi wake kwa sababu yote aliyokuwa akiyafanya hayati Dk. John Pombe Magufuli, alikuwa anayaona. Kikubwa tumpe nafasi na ushirikiano," alisema Mpanju. Aliwataka baadhi ya watu aliowaita wabadhirifu na wenye nia mbaya, kukaa mbali na Rais Samia.

"Ni vyema watu waliozoea mifumo ya ubadhirifu na wizi huko nyuma wasimwingilie katika kazi zake, wasitake kumshawishi, wasitake kumpeleka kwenye kona zao, huyu ni mama yetu ni Rais wetu na ni kiongozi wetu, na ndiye anategemewa na Watanzania kwa sasa," alisema Mpanju.

Kadhalika, alisisitiza baada ya kufariki kwa hayati Dk. Magufuli, matumaini ya Watanzania kwa sasa ni kwa Rais Samia kwa kuhakikisha anaendeleza yale yote yaliyoachwa na mtangulizi wake.

# DC awataka Masasi kumwombea Magufuli

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MKUU wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Selemani Mzee, amewaomba wakazi wa wilaya hiyo kufanya maombi ya heshima ya kumwombea aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kwa lengo la kumkumbuka na kuyaenzi mazuri yote aliyoyafanya wakati wa uhai wake.

Mzee aliyasema hayo mjini Masasi, baada ya kusaini kitabu cha kumbukumbu ya maombolezo ya Hayati Dk. Magufuli, ambapo kimefunguliwa katika ofisi ya mkuu huyo wa wilaya kwa ajili ya kutoa fursa kwa wananchi kusaini ikiwa ni sehemu ya kuungana na Watanzania kumuaga kiongozi huyo.

Alisema kuwa anafahamu kuwa wananchi wa wilaya yake wamesikitishwa na msiba huo kwa vile bado wakazi wa Masasi walitamani kuendelea kuwa nae ili aweze kufanya mambo mengine mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya manufaa ya taifa na kizazi kijacho.

Alieleza kuwa Dk. Magufuli atakumbukwa kwa mambo mengi ya kimaendeleo aliyoyafanya wakati wa uhai wake ukiwamo ujenzi wa vituo vya afya, miradi ya maji, vyumba vya madarasa na miundombinu ya barabara.

halotel

Pumzika Kwa Amani
Dkt. John Pombe Magufuli
1959 - 2021



Kwa niaba ya menejimenti ya Halotel Tanzania, tunatoa salamu za rambirambi kwa Mh. Rais Samia Hassan Suluhu, familia, Serikali na Watanzania kwa ujumla.

Daima Tutakukumbuka

Halotel tanzania | Halotel_Tanzania | haloteltz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII
SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Kamati ya Taifa ya Uongozi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF wanaungana na Watanzania wote kumpa pole Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na familia ya marehemu kwa kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

*Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema. Bwana alitoa na Bwana ametwaa. Jina la Bwana libarikiwe.*

Mkurugenzi Mtendaji
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF**
S.L.P. 2719 Dodoma, Tanzania
Simu: **+255 26 296 3866** Nukushi: **+255 26 296 3871**
Tovuti: **www.tasaf.go.tz** Barua pepe: **info@tasaf.go.tz**



*Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli*
1959 - 2021
*Tutakukumbuka na kukuenzi daima*

TANGAZO


TICTS
Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Kampuni ya Kimataifa ya Kuhudumia Shehena ya Kontena Bandarini (TICTS)
Tunatuma salamu zetu za pongezi kwa
Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
HUTCHISONPORTS
TANZANIA

# Vijiji vyapewa mashine ya kuchakata magogo

**Na Sad Hamdani, LINDI**

SERIKALI kwa kushirikiana na Finland imevipatia vijiji 18 vilivyopo kwenye mpango wa usimamizi na kuhifadhi misitu, wilaya za Nachingwea na Ruangwa, mkoani Lindi, msaada wa mashine itakayotumika kuchakata magogo na mbao yenye thamani ya Sh. 110,000,000.

Mashine hiyo aina ya merold imetengenezwa Finland, imekabidhiwa kwa wana vijiji hivyo, ambavyo havikutajwa majina na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, wakati wa hafla iliyofanyika viwanja vya Shule ya Msingi Likangara mjini Ruangwa.

Wakizungumza na Nipashe baada ya makabidhiano, Edwine Benard Ntakula, Selemani Juma Issa, wakazi wa Kijiji cha Kilimarondo, Nachingwea, Yassini Abdallah na Sultani Seifu (Nandenje) Ruangwa, walizishukuru serikali hizo mbili kwa msaada huo.

Walisema upatikanaji wa mashine hiyo inayotembea itawasaidia kuzalisha mbao kwa wingi na kuongeza thamani ya mazao yanayotokana na rasilimali misitu na kuondokana kutumia teknolojia duni, misumeno ya kusukuma kwa mikono.

Walisema msaada huo umewasaidia kuondokana na tatizo la kutumia misumeno ya kusukuma kwa mkono.

Akitoa maelezo wakati wa makabidhiano hayo, Ofisa Misitu Idara ya Maliasili na Utalii na Mratibu wa Taifa Programu ya FORVAC kuongeza thamani ya mazao ya misitu, Emmanuel Msoffe, alisema mashine hiyo ni mahususi katika kuongeza thamani ya mazao yanayotokana na misitu nchini.

Msoffe alisema mashine hiyo yenye uwezo wa kuchakata mbao zaidi ya 400 kwa siku, itakuwa chini ya uangalizi wa Halmashauri za Nachingwea na Ruangwa.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akizungumza wakati wa kukabidhi mashine hiyo, aliwataka wananchi wa vijiji husika kuhakikisha wanailinda na kuitunza ili iwasaidie kuwaletea tija kwa kuzalisha mbao kwa wingi bila kusahau ongezeko la mapato yatakayotokana na mauzo yake.

# Washindi 'Sherehekea Pesa' wazawadiwa

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI wa wiki ya kwanza wa promo ya 'Sherehekea Pesa'. Ikiwa kama moja wapo ya promo zinazoendelea katika sherehe za kusherehekea miaka 10 ya Tigo Pesa, wamezawadiwa.

Hiyo ni huduma kamili ya kifedha inayohudumia zaidi ya wateja milioni tisa tangu kuanzishwa kwake.

"Kupitia promo hii ya Sherehekea Pesa, Tigo tumejipanga kutoa zaidi ya shilingi milioni 200 kwa washindi wa wiki na washindi wa mwisho wa promo (yaani grand draw winners)," alisema HVC Segment Manager, Mary Ruta wakati wa hafla ya kutoa zawadi za fedha kwa washindi wa promosheni hiyo.

Katika promo ya 'Sherehekea Pesa' wateja wataingia kwenye droo ya wiki ambapo wateja 10 watapata nafasi ya kushinda Sh. milioni moja kila wiki na washindi 10 wa jumla watapata nafasi ya kushinda Sh. milioni 10 kila mmoja katika kampeni itakayodumu kwa wiki 10.

"Pia kutakuwa na bonasi kwa mawakala wa Tigo Pesa ambao wameweka juhudi kuhakikisha wateja wanapata huduma za uhakika kila wakati.

Tunawashukuru kwa kutuamini na kuwa nasi kwa miaka 10 na tungependa kusherehekea mafanikio haya pamoja. Tunaomba uendelee kuwa pamoja nasi kwa miaka 10 mingine na tunaahidi kukupa huduma na suluhisho zenye kuboresha maisha yako ya kila siku," alisema Ruta.

# Ujenzi wa mabweni Chato wapigwa jeki

**Na Mwandishi Wetu**

UJENZI wa mabweni ya shule zote 34 za kata za sekondari wilayani Chato, umeungwa mkono.

Benki ya NMB imekuwa taasisi ya kwanza ya kifedha katika wilaya hiyo mkoani Geita kuunga mkono kampeni ya wilaya hiyo ya ujenzi wa mabweni hayo.

Kampeni hiyo inalenga kuwapunguzia mzigo wanafunzi kwenye shule hizo wapatao 20,678, ambapo wengi wao wanadaiwa kutembea zaidi ya kilometa 25 kila siku kwenda shule na kurudi nyumbani.

Katika kuunga mkono kampeni hiyo benki hiyo imetoa mabati 180 kwa ajili ya ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari Bongera, huku ikitoa pia madawati 110 kwa shule za msingi Ihanga na Kakeneno.

Akipokea msaada huo Mkuu wa Wilaya hiyo, Charles Kabeho, ameishukuru benki hiyo kwa msaada huo, ambapo umeunga juhudi za kuhakikisha lengo la wilaya hiyo linatimia.

Alisema msaada wa mabati utatumika kuezeka bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Bongela ambayo wanafunzi wa kike wamekuwa watoro na wanashindwa kutimiza ndoto yao ya kupata elimu kutokana na umbali.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bongela, Pastory Kihung, alisema wanafunzi wengi wa kike hawamalizi masomo ya kidato cha nne kutokana na utoro unaosababishwa na shule kuwa mbali.

Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladslaus, alisema vifaa hivyo vilivyotolewa thamani yake ni Sh. milioni 12.6 ambapo benki hiyo imetoa ili wanafunzi wa wilaya hiyo wapate elimu katika mazingira bora.


## TAZAMA PIPELINES LIMITED

### CONTAINER DEPOT

### EMPLOYMENT OPPORTUNITY

TAZAMA Pipelines Limited, an interstate organization owned by the United Republic of Tanzania and the Republic of Zambia and which deals in transportation of crude oil from Dar es Salaam to Ndola, Zambia, wishes to invite applications from suitably qualified candidates to fill the below-mentioned post for its new Container Depot at Keko, Dar es salaam.

**1. YARD PLANNER (ONE POST)**

**Job Purpose:** Ensure proper planning of placement and overall movement of containers in liaison with other sections in order to facilitate efficient operations of the company.

**QUALIFICATIONS:**
- Form IV Secondary School Certificate.
- Degree in Logistics and Transport from a recognized Institute/University
- At least three years' work experience in reputable firm.
- Very good command of spoken and written English and Kiswahili language
- Knowledge in ICT

**2. YARD SUPERVISOR (ONE POST)**

Job Purpose: Ensure proper supervision of personnel; and use of equipment for smooth movement of containers in order to facilitate efficient operations of the company.

**QUALIFICATIONS**
- Form Four Secondary Education Certificate.
- Degree in Logistics and Transport or equivalent.
- Three years' work experience in shipping logistics as an added advantage.
- Spoken English and Kiswahili language
- Knowledge in ICT

**3. ASSISTANT YARD SUPERVISOR (ONE POST)**

**Job Purpose:** Assist and ensure proper supervision of personnel; and use of equipment for smooth movement of containers in order to facilitate efficient operations of the company.

**QUALIFICATIONS**
- Form Four Secondary Education Certificate.
- Diploma in Logistics and Transport or equivalent.
- Three years' work experience in shipping logistics as an added advantage.
- Spoken English and Kiswahili language
- Knowledge in ICT

**4. ASSISTANT ACCOUNTANT (ONE POST)**

Job Purpose: Undertake the provision of accounting services in order to facilitate company operating services in order to facilitate company transactions and ensure compliance with accounting policies, company procedures and statutes.

**QUALIFICATIONS**
- Form Four Secondary Education Certificate.
- Degree in Accounts/ Finance or equivalent.
- Three years' work experience.
- Spoken English and Kiswahili language
- Knowledge in ICT

**5. CONTAINER HANDLER/FORKLIFT OPERATOR (THREE POSTS)**

**Job Purpose:** Facilitate efficient movement and stacking of containers in order to ensure efficient operations.

**QUALIFICATIONS**
- Form Four Secondary Education Certificate.
- Certificate in Operations of Reach Stacker equipment/ Forklift from Bandari College.
- Knowledge in Automobile Engineering is an added advantage.
- Three years' work experience.
- Spoken English and Kiswahili language

**6. TALLY/ DATA ENTRY CLERK (FOUR POSTS)**

**Job Purpose:** Ensure accurate counting, inspection and assessment of container quality in order to facilitate efficient operations.

**QUALIFICATIONS**
- Form Four Secondary Education Certificate.
- Diploma in Logistics, Shipping, Accounts or Procurement.
- Two years' work experience in container depots as an added advantage.
- Spoken English and Kiswahili language
- Knowledge in ICT

**7. TRUCK DRIVER (THREE POST)**

**Job Purpose:** Drive company trucks in order to facilitate movement of containers.

**QUALIFICATIONS**
- Form Four Secondary Education Certificate.
- Class C driving license specialized in truck driving.
- NIT certificate in truck driving as an added advantage.
- Three years' work experience in port operations.
- Spoken English and Kiswahili language

**REMUNERATION:**

Attractive remuneration packages will be offered to the successful candidates for the above positions.

**MODE OF APPLICATION:**

Application in own handwriting with detailed CV including photocopies of relevant academic certificates should be submitted to the undersigned within two weeks from the date of this advertisement.

***Only short listed candidates will be contacted.***

**HEAD HUMAN RESOURCE**
**TAZAMA PIPELINES LIMITED,**
**NEAR TUNGI TANESCO**
**KIGAMBONI**
**P O BOX 2157,**
**DAR ES SALAAM.**

Nipashe
Spotika




WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA HARAKA MABAO 20 UEFA UK. 12-13



# MABEKI WA5 BORA WA KUSHOTO EPL

SHAW

**LONDONA,** England

KUNA idadi kubwa ya walinzi bora wa pembeni kwenye Ligi Kuu England, EPL, kwa sasa.

Awali kulikuwa na mjadala kuhusu walinzi bora wa kushoto waliocheza kwenye Ligi Kuu England, huku majina kama Dennis Irwin, Ashley Cole, Patrice Evra na Stuart Pearce yakitajwa.

Makala haya yanakuchambulia walinzi watano bora wa kushoto kwenye EPL msimu huu, tiririka nayo sasa...

**#5. STUART DALLAS**

Dallas amecheza zaidi ya mechi 200 katika nafasi ya beki wa pembeni kutoka kushoto hadi kulia.

Ni mmoja wa wachezaji muhimu sana wa Leeds United na amecheza mechi nyingi zaidi msimu huu akiwa kama beki wa kushoto.

Dallas amekuwa mhimili bora zaidi kwa kikosi hicho cha kocha Marcelo Bielsa na amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho mbili msimu huu.

**#4. KIERAN TIERNEY**

Ni mchezaji wa kimataifa wa Scotland na amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu pale Arsenal. Amekuwa mchezaji ambaye anasaidia kusukumiza mashambulizi mbele kwa 'Washikabunduki' hao.

Tierney ana bao moja na pasi moja ya mwisho kwenye Ligi Kuu msimu huu na akicheza nafasi ya mlinzi wa kushoto.

**#3. LUCAS DIGNE**

Lucas Digne aliumia kifundo cha mguu mwanzoni mwa mwaka huu na alikuwa na wakati mgumu katika kipindi cha kwanza cha msimu huu. Lakini ni mabeki wachache kwenye Ligi Kuu ambao wanaweza kufikia kiwango cha nyota huyo wa Everton.

Digne, mchezaji wa zamani wa Barcelona mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akicheza nafasi ya mlinzi wa kushoto.

Kocha Carlo Ancelotti amekuwa akipenda zaidi kumtumia mara kwa mara Digne kwa sababu ya uwezo wake wa kusaidia mashambulizi.

**#2. AARON CRESSWELL**

West Ham United wamekuwa na kiwango cha kushangaza sana msimu huu. 'Wagonga Nyundo' hao wa London kwa sasa wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, wakipitwa pointi mbili na timu iliyopo nafasi ya nne.

Kocha David Moyes ameimarisha kikosi chake, lakini amekuwa akimtumia zaidi Cresswell mwenye umri wa miaka 27, kama mlinzi wa kushoto.

Cresswell pia amekuwa akichezeshwa kama mlinzi wa kati, kama Moyes akitumia mfumo wa mabeki watatu.

Cresswell kwa sasa ana pasi za mwisho saba kwa jina lake katika mechi 27 alizocheza kwenye Ligi Kuu. Hata akiwa anacheza nafasi ya mlinzi wa kati, amekuwa na uwezo wa kusukumiza mashambulizi mbele.

**#1. LUKE SHAW**

Wakati Luke Shaw alipopenyeza kwenye kikosi cha wakubwa cha Manchester United, alikuwa mchezaji kijana. Amekuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi tangu kuingia kwenye kikosi hicho.

Shaw mwanzo alikuwa na wakati mgumu chini ya kocha Ole Gunnar Solskjaer, lakini sasa ameimarika hasa baada ya ujio wa Alex Telles.


Solskjaer, wakati alipomleta Telles kwenye kikosi chake alileta ushindani zaidi kwa Shaw na hivyo kujikuta 'akiamka' na kupambana kwelikweli na amekuwa mchezaji bora kwenye Ligi Kuu kwa kipindi cha miezi miwili iliyopita.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa katika kiwango bora cha kukaba na kuisaidia vizuri timu yake msimu huu. Manchester United ambayo ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi, Shaw amekuwa mmoja wa mihimili mikubwa ya kikosi hicho.

Hadi sasa kwenye Ligi Kuu England, Shaw amefunga bao moja na kutoa pasi za mwisho tano msimu huu kwa jina lake.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Brazil na Paris Saint-Germain, Neymar ndiye mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi kwa bara la Amerika Kusini [Euro milioni 128] akifuatiwa na Straika wa Argentina na Barcelona, Lionel Messi pamoja na Kipa wa Brazil na Liverpool, Alisson Becker kila mmoja akiwa na thamani ya Euro milioni 80.



## Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIOFUNGA HARAKA MABAO 20 UEFA



HAALAND

**NYON,** Uswisi

ERLNG Haaland aliing'arisha Borussia Dortmund wakati ikifuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa 2020-21, kwa kuonyesha kiwango bora kabisa.

**Raia huyo wa Norway alifunga mara mbili dhidi ya Sevilla nyumbani na kuifanya Dortmund kusonga mbele kwa ushindi wa uwiano wa mabao 5-3, na yeye akifikisha mabao 10 kwa msimu huu.**

Amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga kwa haraka zaidi mabao 20 katika historia ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akifanya hivyo katika mechi 14 tu.

Makala haya yanakuletea wachezaji 10 waliofunga mabao 20 kwa haraka zaidi, twende sasa...

### #10. MARCO SIMONE – MECHI 35

Marco Simone alifunga bao lake la 20 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akipiga 'hat-trick' dhidi ya Sturm Graz mwaka 2000.

Straika huyo wakati wake wa uchezaji alifunga jumla ya mabao 150 kwa timu za AC Milan, Paris Saint-Germain na AS Monaco.

### #9. KARIM BENZEMA – MECHI 34

Karim Benzema alifunga bao lake la 20 la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye mchezo dhidi ya Ajax wakati wakishinda 3-0 mwaka 2011.

Benzema alifunga katika kila msimu kwa misimu 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na anahitaji mabao matatu zaidi kuivunja rekodi ya Raul ya mabao 71 kwenye mashindano hayo.

Straika huyo mkongwe wa Real Madrid alifunga bao hilo la 20 kwenye michuano hiyo katika msimu wake wa saba wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Los Blancos hao.

### #8. JARDEL – MECHI 33

Raia huyu wa Brazil alifunga bao lake la 20 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Galatasaray ikicheza dhidi ya Monaco mwaka 2000.

Mchezaji huyo maarufu kama 'mtu wa safari' amezichezea klabu 18 tofauti na amefunga jumla ya mabao 400 kwenye maisha yake ya uchezaji, yakiwamo 25 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia alimaliza kama mfungaji bora wa mashindano hayo msimu wa 1999-2000, akifunga 10, na kuwa mchezaji wa mwisho wa Galatasaray kupata mafanikio hayo.

### #7. RIVALDO – MECHI 33

Gwiji huyu wa Brazil mabao yake ya kwanza 22 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya yalikuja akiwa Barcelona.

Mchezaji mwingine ambaye alifunga mabao na kushinda mataji muhimu ni Rivaldo, ambaye mafanikio ya Ligi ya Mabingwa Ulaya aliyapata wakati akiwa Barcelona.

Kiukweli mabao yake 22 katika mechi 27 kwenye mashindano hayo alifunga wakati akiwa Barcelona. Bao lake la 20 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya alifunga dhidi ya Olympique Lyon mwaka 2001 kwa mkwaju wa penalti.

### #6. MARIO GOMEZ – MECHI 32

Straika wa zamani wa Ujerumani, Mario Gomez alikuwa mfungaji mzuri ambaye alifunga jumla ya mabao 26 kwenye Ligi ya Mabingwa katika mechi 44.

Mabao yake mengi kwenye mashindano hayo alifunga wakati akiichezea Bayern Munich; na alifunga bao lake la 20 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wakiifunga Basel mabao manne mwaka 2012.

### #5. FILIPPO INZAGHI – MECHI 28

Gwiji wa kweli wa AC Milan, Filippo Inzaghi alifurahia mafanikio akiwa na klabu hiyo kwa kipindi cha miaka 11, akibeba mara mbili taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #4. RUUD VAN NISTELROOY – MECHI 27

Msimu bora wa Ruud van Nistelrooy kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ulikuwa ni wa 2002-03, wakati alipofunga mabao 12 kwenye mechi tisa.

Mchezaji huyo aliacha alama nzuri kwa kila timu aliyoichezea na kuweka rekodi yake kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Amefunga jumla ya mabao 56 kwenye mashindano hayo, akiwa amemaliza msimu kwa kuwa mfungaji bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu mitatu tofauti.

Nyota huyo wa zamani wa Uholanzi alianza kucheza kwenye michuano hiyo wakati akiwa na klabu ya PSV Eindhoven kabla ya kwenda kupata mafanikio Manchester United na baadaye Real Madrid.

### #3. ALESSANDRO DEL PIERO – MECHI 26

Alessandro Del Piero alikuwa mmoja wa wafungaji bora zaidi wa Italia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Del Piero pengine anaweza asiwe na mafanikio makubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini alifanikiwa kwenye ligi ya nyumbani.

Alifunga jumla ya mabao 42 kwenye mashindano hayo katika misimu 15 aliyocheza.

Straika huyo maarufu zaidi Italia alifikisha idadi ya mabao 20 kwenye michuano hiyo katika mechi 26.

### #2. HARRY KANE – MECHI 24

Si tu kwenye Ligi Kuu ya England, Harry Kane pia amekuwa na rekodi ya kuvutia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kane ni mgeni kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwani alianza kwa mara ya kwanza kuicheza mwaka 2016, lakini ameweza kufunga mabao 20 kwenye mashindano hayo.

Zaidi ni kwamba alitumia mechi 24 tu kufunga mabao hayo akiwafunga miamba ya soka la Ulaya kama Juventus, Bayern Munich, Borussia Dortmund na Barcelona.

### #1. ERLING HAALAND – MECHI 14

Tangu alipoanza kucheza kwenye mashindano haya akiwa na Salzburg Septemba mwaka 2019, Erling Haaland amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi kwa ufungaji.


Wakati akifunga mabao mawili kuisaidia Borussia Dortmund kufuzu hatua ya robo fainali, yalimfanya kufikisha mabao 20 katika mechi 14 tu.

Kwa maana hiyo Haaland mwenye umri wa miaka 20 raia wa Norway amezima rekodi za magwiji kama Zinedine Zidane, Francesco Totti, Ronaldo Nazario, Ronaldinho na Radamel Falcao.

Na kwa kuwa bado umri wake mdogo na huku akiwaniwa na klabu nyingi kubwa Ulaya, kuna uwezekano mkubwa wa kuweka rekodi nyingi zaidi kwenye mashindano hayo.

## Nukuu

Mimi kama kiongozi wenu nitafurahi sana siku moja mkiniita hapa kuja kukabidhi Kombe la Afrika lililochukuliwa na timu yoyote katika nchi yetu. Kwa hiyo niwaombe Simba mkawa wa kwanza kuleta Kombe la Afrika hapa Tanzania," **Hayati Rais Dk. John Magufuli, akizungumza enzi za uhai wake wakati akiikabidhi Simba ubingwa wa Ligi Kuu msimu wa 2017/18.**



"Tutakukumbuka [John Magufuli] daima kwa yote mazuri uliyoyapigania na kuyatekeleza katika vipindi vyako vya uwaziri na urais wa nchi yetu. Pole kwa mama Janet [Magufuli] na familia, pole kwa mama Samia [Suluhu] nasi Watanzania. Umeumaliza mwendo mzee wetu, tunakuombea upumzike kwa amani. R.I.P Mr President," **Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta.**



"Kweli kizuri hakidumu. RIP mzalendo wa kweli [Hayati Rais John Magufuli), Mtanzania uliyeiweka Tanzania mbele na sio ubinafsi, naamini wakujifunza tumejifunza mengi sana kutoka kwako na wakuona tumeona mengi sana mazuri kutoka kwako. Wewe ni zaidi ya somo kwa Watanzania," **Nahodha wa Simba, John Bocco.**



# KAULI 5 ZA DK. MAGUFULLI ZA KUKUMBUKWA MICHEZONI




Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, akiwa uwanjani enzi za uhai wake kushuhudia mechi ya Simba na Yanga Machi 8, mwaka jana ambayo ilimalizika kwa Yanga kushinda 1-0. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

TAIFA la Tanzania lipo kwenye simanzi ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17 kwenye Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam. Ni Rais pekee Tanzania ambaye amefariki dunia akiwa bado madarakani.

**Mengi yameandikwa, na mengi yamesemwa kuhusu Rais Magufuli kwenye nyanja mbalimbali. Kwenye makala haya tunamwelezea Hayati Magufuli kuhusu michezo.**

Pamoja na kazi zingine, lakini Dk. Magufuli alikuwa ni mpenda michezo. Akipata muda alikuwa anakwenda uwanjani kuungana na Watanzania wenzake.

Kama itakumbukwa Machi 8, mwaka jana alipokuwa mgeni rasmi kwenye mechi ya Ligi Kuu msimu wa 2019/20, kati ya Yanga na Simba.

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilishinda bao 1-0, lililowekwa wavuni na Bernard Morrison, wakati huo akiichezea timu hiyo, kabla ya kuhamia Simba miezi michache baadaye.

Alionekana pia kufuatilia mambo mbalimbali ya michezo. Alijua vitu vingi kuhusu michezo mbalimbali, kiasi cha kushangaza wengi wanaposimama na kuiongelea.

Leo tutaangalia kauli tano za kukumbukwa kwenye michezo za Dk. Magufuli alizozitoa wakati wa uhai wake, akiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania...

### #1. AWAPASHA MASHABIKI KWA KUNG'OA VITI

Akizungumza na Wahariri wa Vyombo vya Habari mwaka 2016, ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kuingia madarakani, pamoja na mambo mengine, alionyesha kukasirishwa na mashabiki waliodhaniwa kuwa ni wa Simba kwa kung'oa viti kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati huo ukiitwa wa Taifa.

Akasema kuwa pamoja na mambo mengine ya kufanya, anapenda sana michezo, lakini hapendi kuona watu wakivunja viti.

"Napenda michezo, lakini sipendi kuona timu zinang'oa viti. Bora nikaangalie Ndondo Cup kuliko kwenda kuangalia timu zikifungwa zinang'oa viti," alisema Magufuli.

Alisema hayo kutokana na tukio lililotokea Oktoba Mosi, mwaka 2016, Ligi Kuu msimu wa 2015/16, Yanga ilipocheza na Simba kwenye Uwanja wa Taifa.

Ni bao la Mrundi Amissi Tambwe ndilo lililoleta kizaazaa kwani kabla ya kufunga, Tambwe aliutengeneza kwa mkono kabla ya kuuweka wavuni, kitu kilicholalamikiwa na mashabiki wengi wa Simba uwanjani na kuanza kufanya vurugu, hadi pale Shiza Kichuya alipoisawazishia.

### #2. AITAKA SIMBA ITWAE KOMBE LA AFRIKA

Ilikuwa ni Mei 9 kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Mkapa), Rais Magufuli wakati huo alipoitwa kuikabidhi Kombe la Ubingwa wa soka nchini 2017/18.

Katika mechi hiyo, Simba ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar. Hakuridhika na aina ya soka la mabingwa lilivyokuwa linachezwa.

Akasema kabisa kuwa haoni kikosi cha kwenda kupambana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na kuwataka wabadilishe kikosi na kusajili baadhi ya wachezaji wenye uwezo.

"Mimi kama kiongozi wenu nitafurahi sana siku moja mkiniita hapa kuja kukabidhi Kombe la Afrika litakalochukuliwa na timu yoyote katika nchi yetu. Kwa hiyo niwaombe Simba mkawe wa kwanza basi kuleta Kombe la Afrika hapa Tanzania," alisema maneno hayo, baada ya mechi hiyo.

### #3. AIOMBA MOROCCO KUJENGA UWANJA

Mwaka 2016, Rais Magufuli, pamoja na mambo mengi, alimuomba Mfalme wa Morocco kujenga uwanja mkubwa wa kisasa mjini Dodoma.

Akiwa kwenye ziara ya siku tano nchini, Hayati Magufuli aliomba serikali ya nchini humo kuijengea Tanzania uwanja ambao utafanya watu wengi kuendelea kupenda na kufuatilia michezo

"Nimemwomba Mfalme ajenge msikiti mkubwa hapa jijini Dar es Salaam. Lakini nimemwomba atujengee uwanja mkubwa wa mpira Dodoma ambao utagharimu kiasi cha dola milioni 100 ambao utakuwa mkubwa zaidi ya huu wa taifa, vyote amekubali atajenga," amesema Rais Magufuli.

### 4. AIJIA JUU TAIFA STARS KWA KUFUNGWA

Ilikuwa ni Oktoba 2018, alipowaita viongozi wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) na wachezaji wa timu ya Taifa, Taifa Stars Ikulu, Dar es Salaam.

Hiyo ilikuwa ni baada ya ushindi dhidi ya Cape Verde wa mabao 2-0, Stars ikisaka tiketi ya kwenda AFCON iliyofanyika 2019 nchini Misri.

Katika hafla hiyo, Magufuli alionekana kuchukizwa na tabia ya kufungwafungwa ovyo.

"Napenda sana michezo, lakini mimi siyo shabiki wa timu yoyote hapa Tanzania. Sipendi kushindwa, na ni aibu sana watu milioni 55 kushindwa kutinga AFCON," alisema.

### #5. ATANGAZA KUJENGA UWANJA DODOMA

Novemba mwaka jana, Rais Magufuli akiwa kwenye sherehe za kuapishwa aliahidi kujenga uwanja mkubwa jijini hapo kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma.

"Naishukuru na kuipongeza kamati ya maandalizi kwa matayarisho mazuri kwa hakika sherehe imefana sana, kwa sababu watu wamejaa ndani ya uwanja, lakini wamejaa pia nje ya uwanja, hii inanipa changamoto serikali ninayoiongoza na kwamba kitu cha kwanza tutaanza kujenga uwanja mkubwa sana hapa Dodoma, ili sherehe zingine zinazokuja watu wote wa Dodoma waweze kuwa ndani ya uwanja na washerehekee vizuri," alisema.

## JE, WAJUA?



MSHAMBULIAJI wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo, kwa sasa ndiye mfungaji bora wa wakati wote duniani baada ya wiki iliyopita kuivunja rekodi ya mabao 767 iliyokuwa ikishikiliwa na gwiji wa Brazil, Pele, kwa kufunga hat-trick' dhidi ya Cagliari na kufikisha mabao 770 tangu ameanza kucheza soka.





# Wamkumbuka JPM kwa uwezeshaji mikopo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU wa Umoja wa vikundi vya wajasiriamali Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, amesema watamkumbuka Hayati Rais John Magufuli kwa kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya asilimia 10, bila riba inayotolewa na halmashauri kwenye vikundi vya vijana, wanawake na walemavu.

Dioniz aliyasema hayo jijini Dodoma, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu kifo cha Rais Magufuli, kilichotokea Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena mkoani Dar es Salaam.

Alisema, katika kipindi chake cha urais Magufuli alisisitiza vikundi vya vijana, wanawake pamoja na walemavu kupata mikopo ya asilimia 10, kutoka katika halmashauri zao bila riba.

Pia, alisema kabla ya kuingia madarakani utaratibu wa utoaji mikopo ulikuwa hauzingatiwi na halmashauri, hivyo vijana, wanawake pamoja na walemavu walikuwa hawana sehemu ya uhakika ya kupata mikopo.

"Alipoingia madarakani utaratibu wa kutolewa mikopo ulibadilika ambapo sheria ilitungwa bungeni ili kulifanya jambo hili kuwa rasmi, lakini riba iliondolewa kwani hapo awali mikopo hii ilikuwa na riba," alisema.

Aidha, alisema baada ya kutungwa kwa sheria pia walemavu waliingizwa rasmi katika utaratibu huo kama kundi maalum la kupatiwa mikopo hii bila riba.

"Tunamshukuru sana Rais Magufuli kwa hili kwani vikundi vingi vimenufaika na mikopo hii na kusaidia kuongeza ajira kwa vijana na kuondoa utegemezi kwa wahitimu wa vyuo vikuu waliokuwa wakitegemea kuajiriwa na serikali," alisema.

Vilevile, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano kiwango cha mikopo kilipanda ambapo vijana wenye kikundi walikuwa na uwezo wa kukopa kiasi wanachokitaka wenyewe.

"Kwa mfano sisi katika kikundi chetu tulipatiwa mkopo wa Sh. milioni 30, kiasi ambacho hapo nyuma ilikuwa ni vigumu kukipata kwani wakati mwingine kikundi chenye watu 10, kilikuwa kinapatiwa Sh. milioni mbili kiasi ambacho kilikuwa hakitoshi," alisema.

Kadhalika, alisema pamoja na mafanikio hayo pia serikali ya awamu ya tano ilifanikiwa kufanyia marekebisho kwenye utaratibu wa utoaji wa mikopo kwa makundi hayo matatu.

Alisema, marekebisho hayo ni pamoja na kupunguza idadi ya wanakikundi kutoka watu 10, hadi watano na kwa walemavu kuruhusiwa kupata mkopo hata bila kuwa na kikundi.

"Sisi kama wajasiriamali tutaendelea kumwombea kwa Mungu apumzike kwa amani na tunamwombea Rais aliyeapishwa kuchukua nafasi yake Samia Hassan Suluhu Mungu amwongoze ili afuate nyayo zake na kutimiza yale ambayo alikuwa kayapanga mtangulizi wake," alisema Dioniz.



Maandalizi ya eneo la kuuga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Bungeni jana. Wabunge wataaga mwIli huo leo asubuhi kabla ya kupelekwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kuugwa kitaifa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jiji laja na mkakati wa ufaulu sekondari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeanzisha mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuongeza ufaulu kwenye shule zake za sekondari ikiwamo kuwajengea uwezo walimu.

Ofisa Elimu Sekondari wa Jiji hilo, Upendo Rweyemamu, aliyasema hayo kwenye semina ya kuwajengea uwezo walimu hao.

Alisema walimu wa somo moja hukutanishwa kila wiki Ijumaa kuwajengea uwezo.

"Tunafanya hivi makusudi ili kuwapitisha zamani tulikuwa na mafunzo tunaenda ADEM sasa hivi kama vile kuna wimbi hapo katikati tumeona hiyo nafasi izibwe kwa jinsi hiyo," alisema.

Ofisa elimu huyo alisema walimu hao wanapokutana hupewa mafunzo na wataalamu kuanzia asubuhi hadi jioni wakidadavua kwa kina somo husika.

"Tuna mfumo mpya wa mitihani yetu kuanzia mwaka jana kwa hiyo unakuta mwalimu yupo Chihanga, Hombolo yupo peke yake na hawezi kuelewa nini kinaendelea ni vigumu kumtoa mwanafunzi, hivyo unapomkutanisha na wenzake ambao wengine wameshiriki usahihishaji wa mitihani kupitia format hiyo mpya wakikutana na wadhibiti ubora tunawaweka vizuri," alisema.

Rweyemamu alisema kwa sasa wapo kwenye somo la tano na wataendelea kwa masomo yote na kutengeneza kundi ambalo litasaidia kuondoa kero zilizopo kwenye masomo yao.

"Naamini kupitia semina hizi zitasaidia walimu wengine maana tunachukua mwalimu mmoja mmoja kila shule kwa mfano hatuwezi kuchukua mwalimu wa kiingereza wote tunachukua mmoja ambaye akirudi anakaa na walimu wenzake kuwaelekeza," alisema.

Naye Mdhibiti wa Ubora wa Elimu Wilaya hiyo, Lucy Mbolu, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa walimu kwa kuwa ubora unatakiwa uzingatiwe kwenye ufundishaji.

# Walimu elimu awali Kongwa, Chamwino waongezewa uwezo

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

SHIRIKA linalojishughulisha na malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (CiC), limeongeza uwezo wa walimu wa awali katika Wilaya za Kongwa na Chamwino kumudu mbinu za ufundishaji wa elimu ya awali kutoka asilimia 50 hadi 70.

Akizungumza na Nipashe, mratibu wa mradi wa miaka mitatu wa 'Watoto wetu tunu yetu' unaotekelezwa na CiC katika wilaya hizo, Frank Samson, alisema ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya awali ulikuwa asilimia 50 kwa mwezi Aprili 2020 na umeongezeka na kufikia asilimia 70 ilipofika Desemba mwaka jana.

Alisema matokeo hayo yametokana na tathmini fupi iliyofanywa ndani ya mradi huo baada ya walimu hao kupatiwa mafunzo.

"Kabla ya mradi kulikuwa na vitu vingi ambavyo vilikuwa vikwazo kama vile mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa darasa la awali ambavyo walimu walikuwa hawajui ikiwamo kulifanya darasa kuwa changamshi lakini baada ya mafunzo walimu wameongeza uwezo katika eneo

hilo na hivyo kuanza kuleta tija kwa darasa," alisema. Mratibu huyo alisema hivi sasa kuna madarasa changamshi yenye zana mbalimbali zinazotokana na mazingira kwa shule 232 za Kongwa na Chamwino, hivyo kuwafikia watoto 22,000 wa elimu ya awali kufikia Februari mwaka huu.

Kuhusu ongezeko la uelewa, alisema uelewa wa elimu ya awali umeongezeka kutoka asilimia 28 mwezi Aprili mwaka 2020 hadi asilimia 65 Desemba mwaka 2020.

"Mafunzo yamesaidia kuongeza ushiriki wa wazazi na jamii kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya awali ikiwamo ushiriki wao katika kutengeneza zana na utoaji wa lishe kwa watoto," alisema.

Alibainisha katika mradi huo kwa kushirikiana na serikali wamegawa vitabu vya watoto 42,000 vya kujifunzia wakiwa nyumbani pamoja na vitendea kazi vyake.

"Pia kwa kushirikiana na serikali tumefanikiwa kuweka mifumo ya maji ya kunawa mikono kwa shule 46 zilizopo Chamwino na Kongwa," alisema.



## Waomba wadau kusaidia ujenzi shule ya msingi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa Mtaa wa Gombe Kaskazini, Kata ya Isyesye, jijini hapa wamewaomba wadau kujitokeza kusaidia ujenzi wa Shule ya Msingi Mafanikio ili kuwaondolea adha wanafunzi wanaotembea umbali wa zaidi ya kilometa tatu kwenda shuleni.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Gombe, Christopher Mwaitege, alisema kutokana na adha kubwa wanayoipata wanafunzi hao, wananchi walikubaliana kutumia nguvu kazi zao kujenga madarasa matatu kwa kuanzia huku waliendelea kutoa michango ili kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa shuleni hapo.

Alisema shule hiyo ya Mafanikio ni mpya ilianzishwa kwa lengo la kukabiliana na adha ya watoto kutumia umbali mrefu kwenda shule nyingine.

"Viongozi wa mtaa na wananchi tulikubaliana kwa pamoja kujitoa kwa hali na mali kuanza ujenzi wa shule hiyo mpya ili kuwasaidia watoto kusoma karibu badala ya kutumia umbali wa kilomita tatu kwenda shule muitiko ni mzuri hadi sasa madarasa matatu yanakamilika ombi letu ni wadau kutusaidia kujenga madarasa mengine," alisema Mwaitege.

Mstahiki Meya Jiji la Mbeya, Dour Mohammed, aliahidi kushirikiana na wananchi kukamilisha shule hiyo alisema atahakikisha anakuwa bega kwa bega katika kuhakikisha kuwa shule hiyo inakamilika mapema.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, aliahidi kushirikiana na wananchi hao na kutoa kokoto na mifuko 60 ya saruji.

Alisema kukamilika kwa shule hiyo ya msingi kutakuwa ni mafanikio makubwa kuondoa msongamano kwa watoto kukaa darasani na kuondoa adha ya watoto kutembea umbali mrefu.

# Taasisi ya Tulia yatoa mkopo wa bodaboda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust ametoa mkopo wa bodaboda sita zenye thamani ya Sh. milioni 13 kwa umoja wa madereva ikiwa ni mwendelezo wa uwezeshaji vijana kiuchumi na kujiajiri.

Dk. Tulia alikabidhi bodaboda hizo hivi karibuni kwenye ofisi za umoja huo, Kanda ya Sae, jijini Mbeya na kutumia fursa hizo kuwaasa vijana kuwa waaminifu ili vijana wengine waweze kukopeshwa. Alisema hadi sasa asilimia 90 ya waendesha bodaboda jijini Mbeya wamenufaika na mikopo ya Tulia Trust na wengine wameajiri na kuongeza vyombo vya usafiri. "Mmekuwa mfano wa kuigwa kwa vijana wengine maana mmekuwa waaminifu katika kurejesha mikopo mmehamasisha na wengine kujiunga kwenye vikundi vya bodaboda ili wapate mikopo hiyo," alisema Dk. Tulia. Aliwataka vijana kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kujiletea maendeleo na kuacha kupoteza muda kwenye mambo yasiyokuwa na maana.

Baadhi ya wanufaika wa mkopo wa bodaboda, Agness Legembo, aliwahamasisha kujiingiza kwenye shughuli za bodaboda kwa kuwa inalipa.

Alisema tangu aanze kuendesha bodaboda mwaka 2009 amejenga nyumba, kusomesha watoto na kufungua biashara nyingine za kujiongezea kipato.

Aliwashauri wanawake kutochagua kazi zikiwamo za bodaboda akitoa ushuhuda kwamba imemlipa kwa kuwa amejikwamua kiuchumi.

"Hii ni bodaboda yangu ya pili kwangu kuchukua kama mkopo ambapo ya kwanza nilimaliza vizuri hii niliyochukua tena nitamaliza vizuri sababu najiamini na kazi yangu," alisema Agness.

Mwenyekiti wa Bodaboda Jiji la Mbeya, Aliko Fwanda, alisema ataendelea kuwasimamia vijana ili waweze kurejesha kwa uaminifu mikopo na wengine waweze kukopa.

# H'mashauri zatakiwa kuanzisha klabu upandaji miti

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

HALMASHAURI za miji, wilaya na majiji nchini, zimeshauriwa kuanzisha klabu za upandaji miti kwenye jamii hasa kwenye shule za sekondari na vyuo ili kuwajengea vijana utamaduni wa kupanda miti ili kuongeza ufanisi wa utunzaji wa mazingira.

Ushauri huo ulitolewa juzi na wadau wa mazingira wakati wa uzinduzi wa upandaji wa miti wilayani Rungwe ambao ulifanyika katika chanzo cha maji cha Msasani, mjini Tukuyu.

Ofisa Tawala wa Wilaya ya Rungwe, John Boya, alisema baadhi ya wananchi hawana utamaduni wa kupanda miti kwa sababu hawakujengwa tangu wakiwa wadogo.

Alisema pamoja na kuanzisha klabu hizo, pia elimu ya upandaji miti inatakiwa iendelee katika ngazi zote nchini ili Watanzania wote wawe na uelewa wa upandaji miti na faida zake.

"Nashauri wataalamu wa halmashauri zote nchini wakiona hili jambo linatekelezeka walifanyie kazi, tusiishie tu kutoa elimu kwa watu wachache, ikiwezekana tushuke mpaka ngazi za chini kabisa," alisema Boya. Mwakilishi wa Shirika la Uhifadhi wa Mazingira (WCS), Faraja Dembe, ambao ndio waliondaa upandaji miti, alisema shirika hilo limeandaa miti zaidi ya 100,000 kwa ajili ya kuipanda kwenye maeneo mbalimbali ya vyanzo vya maji.

Alisema watahakikisha wanashirikiana na wadau wengine kupanda miti kwenye vyanzo vyote vya maji vilivyopo wilayani Rungwe na katika maeneo mengine ya Nyanda za Juu Kusini yenye uhitaji.

"Leo tunazindua hapa, lakini tutaendelea kupanda miti hii kwenye vyanzo vingine vya maji, tumeandaa miti tofauti ya matunda na ya asili ambayo yote itapandwa kwenye maeneo tutakayoainisha," alisema Dembe.

TANESCO

HONGERA

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan

Kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



TUNAKUTAKIA MAFANIKIO KATIKA KUIONGOZA TANZANIA

tanesco_official_page
umemeforum.blogspot.com
tanescoyetultd
tanescoyetu



# TAMWA yampongeza Rais Samia Suluhu Hassan

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Wahabari Wanawake Tanzania, upande wa Zanzibar (TAMWA), kimempongeza Samia Suluhu Hassan, kuwa Rais wa awamu ya sita wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania na Afrika Mashariki kushika nafasi ya hiyo.

Samia ameshika nafasi hiyo kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania Dk. John Magufuli, Machi 17, mwaka huu.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema kuapishwa kwa Samia kuwa Rais wa Tanzania kutaweka mustakbali mpya kwa maendeleo ya jinsia nchini pamoja na Afrika Mashariki na kwamba kutatoa nuru zaidi kwa wanawake na wasichana kupaa ngazi za uongozi.

Dk. Mzuri aliwataka Watanzania kuondoa mawazo mgando kuwa hawaamini kwamba wanawake wanaweza kushika nafasi za juu.

Alisema TAMWA ina muunga mkono rais pamoja na kumuomba aandae wanawake zaidi kwenye nafasi za uongozi.

"TAMWA Zanzibar inamtakia kila la kheri Mama Samia katika kipindi chake hiki kizito kutokana na kifo cha aliyekuwa mkuu wake wa kazi na majukumu haya ya kuiendesha nchi katika nafasi ya juu kabisa," alisema.

Dk. Mzuri alisema Mungu amjaalie Mama Samia aongoze kwa hekima, ushirikishaji, uadilifu na kuinua haki za wanawake na haki za binadamu kwa ujumla.

Katika hatua nyingine mke wa Makamu wa Pili wa Rais mstaafu, Mama Asha Suleiman Idd, amewataka wanawake nchini kumpa ushirikiano wa kutosha Rais Samia Suluhu Hassan, atimize majukumu ya kiwajibu na kisera bila kujali itikadi za kisiasa.

Pia alisema kiu ya miaka mingi ya wanawake duniani kufikia ndoto za kushika madaraka ya uongozi wa juu katika nchi zao hususan barani Afrika sasa zimetimia.

Alisema juhudi kubwa zimefanyika na wanawake baada ya kukandamizwa na mifumo dume ili kupata nafasi katika ngazi za uwakilishi na utawala.

Alisema kitendo cha kuapishwa kikatiba kwa mwanamama huyo na kupewa dhamana ya kuliongoza taifa si fahari yake pekee bali ni tunu ya wanawake wote nchini.

Aliwahimiza wanawake kusimama pamoja na kuzidisha mapambano dhidi ya ubaguzi wowote wa kijinsia hatimaye wanawake waishi bila kuonewa na kubaguliwa.

Alisema ni wakati muhimu kwa wanawake wa Afrika Mashariki na Afrika kumpa ushirikiano kwa kuwa ni matokeo chanya baada ya juhudi za wanaharakati, viongozi na wanasiasa walioko kwenye vyombo vya uwakilishi.




Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Karume, akisaini kitabu cha maombolezi ya Hayati Dk. John Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipowasili katika ofisi za CCM Mtaa wa Lumumba kuhudhuria Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa. **PICHA: IKULU**

# Ukosefu elimu chanzo migogoro ya vikundi

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

UKOSEFU wa elimu ya uongozi na utawala bora kwenye vikundi vya ujasiriamali husababisha vikundi vingi kukumbwa na migogoro na kushindwa kufikia malengo yake.

Hayo yalielezwa na Bakar Omar Ali, Ofisa sheria kutoka Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakati wa mafunzo ya uongozi na utawala bora kwa wakulima na viongozi wa vikundi kisiwani Pemba, kupitia mradi wa viungo, mboga na matunda unaotekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Zanzibar (TAMWA- Zanzibar), People's Development Forums (PDF), na Community Forests Pemba (CFP), kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema licha ya wadau kujitahidi kuchukua juhudi kubwa kuhamasisha wananchi kujiunga na vikundi kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi, lakini bado vikundi hivyo vimekuwa vikikabiliwa na migogoro ya hapa na pale ambayo chanzo chake kikubwa ni ukosefu wa misingi ya utawala bora ndani ya vikundi hivyo.

Alisema suala la uongozi bora kwenye vikundi ni muhimu katika ustawi wa maendeleo ya wanawake hasa wanachama wa vikundi hivyo ili kutimiza malengo ya uanzishwaji wa vikundi.

"Vikundi vingi vinaanzishwa kila siku, lakini havidumu kutokana na kukosekana kwa misingi hii ya utawala bora, na ukifuatilia migogoro mingi inayojitokeza kwenye vikundi chanzo chake utakuta ni ukosefu wa viongozi bora," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo kuna haja kwa wadau wa maendeleo kuongeza nguvu katika utoaji wa taaluma ya uongozi na utawala bora kwenye vikundi hivyo ili kufikia malengo ya kuwasaidia wananchi kujiendeleza kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali katika jamii. "Tuwapongeze wasimamizi wa mradi huu wa viungo kwa kuliona hili na kuamua kuja na mafunzo haya kwa wanufaika wa mradi huu kwani hii itasaidia kuondoa migogoro ndani ya vikundi inayosababisha vikundi kufa na kushindwa kufikia malengo ya kuanzishwa kwake."

Alisema ujio wa mradi huo utasaidia kutatua changamoto zinazowakabili wakulima hasa wanawake kupitia vikundi vya ujasiriamali na hatimaye kuvifanya vikundi hivyo kuwa ni mkombozi kwao. "Wanawake wengi ambao kwa kiwango kikubwa ndio wanajishughulisha na vikundi wamekuwa wakishindwa kupata mafanikio sahihi ya kujikwamua kiuchumi kupitia vikundi vyao kutokana na vikundi vingi kukosa misingi imara ya uongozi katika kusimamia shughuli zao hivyo mbinu hii ya mradi huu itarejesha matumaini ya wanawake katika vikundi vyao," alisema.

Naye Ofisa uwezeshaji wanawake kiuchumi wa mradi huo, Asha Mussa Omar, alisema mafunzo hayo yamekuja baada ya mradi kugundua kwamba vikundi vinashindwa kudumu na kufikia malengo kutokana na ukosefu wa uongozi imara na kwamba taaluma hiyo itawasaidia kutambua misingi ya utawala bora katika uendeshaji wa vikundi vyao. Alisema malengo ya mradi ni kuwawezesha wanawake kujiinua kiuchumi kupitia shughuli za kilimo cha mboga, viungo na matunda hasa kupitia bustani ya nyumbani pamoja na uwekaji wa hisa na kwa asilimia 55. Mshiriki wa mafunzo hayo, Fatma Shaame, alipongeza uamuzi wa mradi kutoa taaluma hiyo na kuwa tatizo hilo limekuwa kilio chao kwa muda mrefu jambo linalosababisha wananchi wengi kukata tamaa ya kujiunga na vikundi hivyo.

"Tatizo la kuvunjika kwa vikundi chanzo chake ni viongozi kukosa uwajibikaji na hii inatokana kwamba kwenye vikundi tunachaguana bila kujali misingi ya utawala bora. Tunashukuru mradi kuja na fursa hii kwa kuwa sasa itaenda kuimarisha vikundi vyetu," alisema.

# Wananchi wapewa tahadhari mvua ya masika

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wametakiwa kuchukua tahadhari ya maeneo yenye viashiria vya maafa ili kupunguza athari hasa katika msimu huu unaotarajiwa kuanza mvua ya masika.

Mkuu wa Divisheni ya Mawasiliano na Tahadhari kutoka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Omar Ali Mohamed, alisema hayo alipofanya ziara katika Shehia za Wilaya ya Kaskazini A Unguja.

Aliwataka wajumbe wa kamati ya kukabiliana na maafa ya shehia kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kushirikiana na jamii kusafisha mazingira yanayowazunguka ikiwamo mitaro pamoja na kuziondoa changamoto zenye viashiria vya maafa katika maeneo yao.

Aliwaambia wajumbe hao kutoa elimu katika ngazi za familia hasa wale wanaoishi mabondeni jinsi ya kujiandaa mapema kabla ya mvua ya masika haijaanza kushamiri.

"Iwapo eneo unaloishi kila msimu wa mvua za masika huingia maji ni wakati sasa wa kujitayarisha mapema kwa kuondoa vitu vyako vya thamani ili usijepata hasara," alisema.

Naye Ofisa Operesheni na Haki za Binadamu kutoka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Jabu Sharifu, aliwataka wajumbe hao kutoa taarifa katika mamlaka husika yanapotokezea maafa ili kupatiwa msaada wa haraka.

Alisema majanga ya maafa ni mtambuka kwa sababu yanamgusa kila mtu na kwamba iko haja kuyaondoa kwa yale yanayosababishwa na binadamu ili kupunguza vifo na upotevu wa mali.

"Kinamama wenzangu mvua ya masika inakuja mhakikishe watoto wadogo wasiachiwe kwenda shule peke yao kwa kuepuka kuingia kwenye mashimo yanayojaa maji pamoja na vivuko katika mitaro," alisema.

Vile vile, alisema kamisheni ya kukabiliana na maafa imetoa namba ya dharura kwa wale watakaopata maafa ambayo ni 190, kwa msaada wa haraka.

Ziara hiyo ya kukutana na Wajumbe wa Kamati ya Sheha ya Kukabiliana na Maafa Kishehia imefanyika Mkoa wa Kaskazini Unguja na inatarajiwa kuendelea Mkoa wa Kusini Unguja pamoja na Mkoa wa Mjini Magharibi maeneo yanayolengwa ni sehemu ambazo zinaviashiria vya maafa kwa kila mwaka.

## HABARI PICHA



Vijana wa Skauti wakimsaidia mmoja wa waombolezaji. **MPIGAPICHA WETU**



Mlezi Kamati ya Amani Mkoa wa Mwanza, Altaf Hiran Mansoor, akitia saini kitabu cha maombolezo ofisi ya Mkuu wa Mkoa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Rais mstaafu wa Zanzibar ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akisaini kitabu cha maombolezi ya Hayati Dk. John Magufuli alipowasili katika ofisi ya CCM Lumumba kuhudhuria Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kilichofanyika juzi. **PICHA: IKULU**



Mkazi wa Dar es Salaam akisaidiwa baada ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wakazi wa Dar es Salaam wakilia baada ya kutoa heshima zao la mwisho jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkazi wa Wilaya ya Masasi, Adof Bwakila, akiwa amejitokeza jana viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Masasi, kusaini kitabu cha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## HABARI KIMATAIFA

# Utafiti: AstraZeneca chanzo damu kuganda

**Bonn,** UJERUMANI

WANASAYANSI katika hospitali ya mafunzo ya Chuo Kikuu cha Greifswald, wamedai wamegundua kisababishi cha kuganda kwa damu, miongoni mwa watu wachache waliopokea chanjo ya Astrazeneca.

Watafiti kutoka hospitali ya mafunzo ya chuo hicho, kilichopo Kaskazini mwa Ujerumani, walisema mwishoni mwa wiki kuwa waligundua chanzo cha kuganda kwa damu kusiko kwa kawaida, miongoni mwa baadhi ya wapokeaji wa chanjo ya virusi vya corona.

Taarifa hiyo ni baada ya kituo cha utangazaji cha umma cha Norddeutscher Rundfunk (NDR), kuripoti.

Uchunguzi ulionesha namna chanjo hiyo ilivyosababisha mvilio usio wa kawaida kwenye ubongo katika idadi ndogo ya wagonjwa.

**Ugunduzi wa Greifswald haujachapishwa bado katika jarida ya kisayansi na hivyo haujapitiwa na wataalamu huru.**

Ugunduzi huo unamaanisha kwamba tiba makhsusi inaweza kutolewa kwa wale wanaokabiliwa na mvilio sawa, kwa kutumia dawa ya kawaida sana.

Mafanikio hayo yalikuwa matokeo ya ushirikiano kati ya Hospitali ya Greifswald, mamlaka ya afya ya jimbo Taasisi ya Paul Ehrlich (PEI), pamoja na madaktari wa nchini Austria, baada ya muuguzi kufariki kutokana na mvilio katika ubongo baada ya kudungwa chanjo ya AstraZeneca.

Watafiti walisisitiza kwamba tiba itawezekana tu miongoni mwa wagonjwa ambako mgando wa damu unaonekana, kuliko kuwa kama tiba ya kuzuwia. Taarifa hizo zilitolewa kwenye hospitali zote barani Ulaya.

Dalili kama vile maumivu ya mara kwa mara ya kichwa, kisunzi au kupungua kwa uwezo wa kuona zinazodumu kwa zaidi ya siku tatu baada ya kuchanjwa zinahitaji uchunguzi zaidi wa kitabibu.

Kwa mujibu wa chama cha utafiti cha Ujerumani kwa ajili ya mvilio, katika taarifa kuhusu ugunduzi huo wa karibuni. Ugunduzi wa Greifswald haujachapishwa bado katika jarida ya kisayansi na hivyo haujapitiwa na wataalamu huru.

Taasisi ya Paul Ehrlich nchini Ujerumani sasa inapitia kazi hiyo ya wanasayansi. Ujerumani, pamoja na mataifa kadhaa ya Umoja wa Ulaya, yalisitisha matumizi ya chanjo ya AstraZeneca kufuatia ripoti za mvilio usio wa kawaida wa damu.

Wiki iliyopita, mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa dawa ya Umoja wa Ulaya EMA, ilisema hakukuwa na uhusiano uliyothibitishwa kati ya chanjo na mvilio wa damu, kwa msingi wa taarifa walizokuwa nazo.

Walibainisha pia kwamba manufaa ya chanjo hiyo yanazidi uwezekano wowote wa hatari. Katika kujibu mwongozo huo mpya, Ujerumani ilipanga kuanza tena kutoa chanjo hiyo ya Uingereza na Sweden mwishoni mwa wiki.

Ujerumani ilikuwa imekwishatoa zaidi ya dozi milioni 10 za chanjo ya Covid-19, ikiwamo ya AstraZeneca. **DW**



Lori likipita kwenye barabara iliyojaa maji, mjini Old Pitt, Kaskazini Magharibi mwa Sydney nchini Australia jana. Nchini humo hususan mji maarufu wa New South Wales, ulikumbwa na mafuriko ambayo hayajashuhudiwa muongo mmoja uliopita. **PICHA: AP**

## Thailand yakana kugawa mchele Myanmar

**Bangkok,** THAILAND

JESHI la Thailand limekanusha kutoa mchele kwa vikosi vya jeshi la Myanmar na kusema kuwa chakula chochote kinachopelekwa kupitia mpaka wa Myanmar ni sehemu ya biashara ya kawaida.

Vyombo vya habari vya Thailand viliripoti kwamba jeshi la Thailand limetoa magunia 700 ya mchele kwa jeshi la Myanmar kwenye mpaka wa Mashariki mwa Myanmar, vikimnukuu ofisa usalama ambaye hakutambulika akisema walikuwa wanafuata maagizo ya serikali ya Thailand.

Kamanda wa kikosi cha Naresuan, Meja Jenerali Amnat Srimak, alikanusha katika taarifa kuwapo na mawasiliano yoyote na jeshi la Myanmar, likiomba msaada wowote kutoka kwao, kwa sababu wana heshima yao.

Hata hivyo vyombo vya habari vya Thailand, vilionyesha picha za kile kilichoonekana kuwa magunia ya mchele yakipakiwa kwenye malori mpakani. **DW**

## Sanamu ya Donald Trump yaondolewa makumbusho



**New York,** MAREKANI

SANAMU la Donald Trump, limeondolewa kwenye jumba la kumbukumbu baada ya kushambuliwa na kuharibiwa.

Lilikuwa limewekwa kwenye jumba la makumbusho la San Antonio, lililazimika kuondolewa baada ya kushambuliwa mara nyingi.

Kulingana na ripoti ya San Antonio Express-News, maofisa wa Jumba la makumbusho la Louis Tussaud, waliamua kuliondoa sanamu hilo, ambalo lilikuwa likipigwa ngumi kila wakati na kuharibiwa na wageni.

Clay Stewart, mmoja wa maofisa wa jumba la makumbusho, alisema kwamba walikuwa na shida za mara kwa mara dhidi ya sanamu ya wanasiasa mashuhuri na kudhihirisha kuwa mashambulizi ya sanamu la Trump yaliongezeka wakati wa kampeni za uchaguzi mnamo mwaka jana.

Sanamu la Trump lilikuwa likionyeshwa kati ya sanamu za kiongozi wa Urusi Vladimir Putin na kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong-Un.

Stewart alisema kuwa kwa sasa, sanamu la Rais wa Marekani Joe Biden, inaendelea kujengwa na hawana mpango wa kuonyesha tena sanamu la Trump.

Sanamu za marais wengine wa zamani wa Marekani kama vile George W. Bush na Barack Obama pia ziliwahi kushambuliwa na wageni hapo awali. **TRT**




# MOYES AKUNWA LINGARD KUITWA KIKOSINI ENGLAND

**LONDON,** England

KOCHA wa West Ham United, David Moyes, anaamini kuitwa kwa mchezaji wake, Jesse Lingard kwenye kikosi cha timu ya Taifa England haikuwa bahati mbaya, kwani imetokana na kiwango kikubwa alichokionyesha akiwa na 'Wagonga Nyundo' hao wa London.

Tangu ajiunge Januari kwa mkopo na West Ham United akitokea Manchester United, hiyo imekuwa mara ya kwanza kwa winga huyo kupata shavu la kuitwa timu ya taifa ndani ya miaka miwili.

Winga huyo ambaye alikuwa akicheza kikosi cha kwanza cha timu ya Taifa England wakati wa Kombe la Dunia 2018, amerejea kikosini baada ya kutupia mabao manne akiwa na West Ham ambayo inapigania kumaliza katika nafasi nne bora ili msimu ujao ishiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nimefurahishwa na Jesse, amekuwa kwenye kiwango bora, ambacho kimekuwa kikiipa uhai mkubwa timu, nategemea kuona makubwa zaidi kutoka kwake," alisema kocha huyo wa zamani wa Man United akinukuliwa na Sky Sport.

Akizungumzia uwezekano wa kumsajili moja kwa moja baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika, kocha huyo alisema, "tunaweza kuliangalia hilo mwishoni mwa msimu, lakini kwa sasa atabaki kuwa mchezaji wetu ambaye tupo naye kwa mkopo."

# Neymar atabiriwa kucheza tena na Messi

**BARCELONA,** Hispania

NEYMAR ataungana tena na Lionel Messi pale Camp Nou, kwa mujibu wa wakala wa zamani wa Brazil na skauti wa zamani wa Barcelona, Andre Cury.

Cury alitumia muda wa miaka 10 kufanya kazi na Barcelona akiwa kama wakala wao nchini Brazil na alifanya kazi kubwa katika uhamisho wa Neymar kutua Barcelona.

Baada ya kushirikiana na Messi msimu wa 2014-15 na 2015-16, ambao Barca ilishinda LaLiga pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya na Copa del Rey (Kombe la Mfalme), Neymar aliondoka na kwenda Paris Saint-Germain mwaka 2017.

Lakini sasa Cury amesema wawili hao wanaweza kuungana tena katika kikosi cha Barcelona.

Messi amekuwa akihusishwa na kuihama Barcelona, na klabu zinazohusishwa naye ni PSG na Manchester City, lakini Cury anasema anahisi wawili hao wanaweza kuwa pamoja pale Catalunya.

"Miaka miwili iliyopita Neymar aliniomba anataka kurejea Barcelona tulijaribu na tulikuwa karibu kukamilisha mpango huo," alisema Cury akiiambia El Litoral.

"Mtu pekee anayeweza kuwaunganisha tena wachezaji hao ni Rais mpya wa Barcelona, Joan Laporta, Messi hataki kuondoka tena Barcelona ameamua maisha yake na historia yake iwe pale.

"Neymar atacheza tena na Messi, lakini itakuwa Barcelona."







# *Guardiola hajutii Sancho kuondoka*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guadiola, amesisitiza kwamba, hana majuto yoyote kuhusu kuondoka kwa Jadon Sancho mwaka 2017 na kujiunga na Borussia Dortmund.

Sancho alihamia Man City Machi 2015 akiwa na umri wa miaka 14 na haraka sana alipata umaarufu.

Lakini kutokana na sababu mbalimbali alikosa nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza cha City, na Sancho aliuzwa kwa kitita cha pauni milioni nane na sasa amekuwa mmoja wa wachezaji nyota kule kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

"Nilishasema mara nyingi kwamba sijutii, aliamua na anafanya vizuri sana kwa kweli," alisema Guardiola baada ya timu yake kupangwa na Dortmund katika hatua ya robo fainali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nampongeza ni mchezaji wa kipekee, ni mchezaji wa timu ya taifa mwenye kiwango kikubwa anafanya vizuri sana Dortmund."

Sancho ambaye atatimiza umri wa miaka 21 wiki hii, amekuwa nyota kwenye kikosi hicho. Kiwango hicho kimemfanya aitwe katika timu ya taifa na kumuona mara nyingi akihusishwa na uhamisho wa fedha nyingi kurejea kwenye Ligi Kuu England.

# Solskjaer: Tupo kwenye mazungumzo na Cavani

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amethibitisha kwamba klabu hiyo ipo kwenye mazungumzo ya kujadili mkataba mpya na Edinson Cavani.

Cavani alijiunga na United akiwa mchezaji huru mwanzoni mwa msimu huu na nyota huyo mwenye umri wa miaka 34, amekuwa na kiwango cha kuvutia hapo Manchester, ambapo raia huyo wa Uruguay akiwa amefunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho mbili kwenye mechi 25 alizocheza katika mashindano yote.


Mfungaji huyo wa wakati wote wa Paris Saint-Germain, Cavani amekuwa akihusishwa na kwenda kwa miamba wa soka la Argentina, Boca Juniors kutokana na kauli ya baba yake Luis.

Lakini Solskjaer amesema United ambayo ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu – wapo kwenye mazungumzo na Cavani kuhusu majaliwa yake hapo Old Trafford.

"Tunazungumza na Eddy," alisema Solskjaer kabla ya mchezo wa jana Jumapili wa robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Leicester City.

"Edinson ni straika wa daraja la juu na chochote anachoamua anafanya, ngoja tuone. Tupo kwenye mazungumzo mazuri naye.

"Tunataka kikosi cha ushindani na tunahitaji watu pale mbele kwa ajili ya kufunga mabao. Hivyo tunaliangalia hilo."







# KANE ASIKITISHWA NA KIWANGO TOTTENHAM

**LONDON,** England

HARRY Kane amesema hana "maneno ya kusema" kwa wiki mbaya kwa Tottenham Hotspur.

Spurs walianza kufungwa na majirani zao wa Jiji la London, Arsenal kwenye ligi wikendi iliyopita, huku wakitolewa hatua ya 16-bora kwenye Ligi ya Europa na Dinamo Zagreb.

Spurs walikuwa na nafasi ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo, kwani mchezo wa kwanza walishinda mabao 2-0, lakini wiki hii wakajikuta wakiangukia pua baada ya kukubali kipigo cha 3-0 kwa mabao ya Mislav Orsic.

Kane ambaye amefunga mabao matano katika mechi tatu za Ligi Kuu zilizopita, amebainisha kiwango cha hivi karibuni cha Tottenham kinakatisha tamaa.

Nahodha huyo wa England alisema: "Ni muda wa kurudi kwenye kiwango chetu, maana hali ilivyo inasikitisha.

"Kwa sasa sina maneno ya kusema, kwani hali yenyewe inaonekana namna ilivyo kwa kikosi chetu. "Lazima tufanye kazi ya ziada, vinginevyo mambo yanaweza kuwa magumu sana kwa upande wetu."

Tottenham wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, wakipitwa pointi sita na Chelsea waliopo nafasi ya nne, ingawa 'Blues' hao wamecheza mechi nyingi zaidi.

# *Guardiola afurahia mafanikio Man City*

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anaamini kiwango cha Manchester City kwa kipindi cha miezi minne iliyopita ni moja ya "mafanikio makubwa" tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2016.


City walipata ushindi wa 2-0 dhidi ya Everton pale kwenye dimba la Goodison Park Jumamosi na kutinga nusu fainali ya Kombe la FA kwa msimu wa tatu mfululizo – mara ya kwanza kupata mafanikio kama hayo ilikuwa kati ya msimu wa 1931-32 na 1933-34.

Matokeo hayo yameweka rekodi mpya kwa klabu hiyo kwa kucheza na kushinda mechi 17 mfululizo ugenini, ikivunja rekodi yake ya awali iliyowekwa kati ya Januari na Septemba mwaka 1999.

Tangu City ilipopokea kipigo kutoka kwa Tottenham Novemba 21, wameshinda mara 29 kati ya mechi zao 33 kwenye mashindano yote, ikipoteza mara moja dhidi ya majirani zao Manchester United kwenye mchezo wa Ligi Kuu mapema mwanzoni mwa mwezi huu.

Na Guardiola ameonyesha kuridhika na kiwango cha kikosi chake na kuonyesha tofauti.

"Tunatakiwa kuzoea hili; kila mchezo ni tofauti," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi pale Goodison Park.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI Y... YA




# ZIDANE ASHANGAZWA NA UFARANSA KWA BENZEMA

●●● Huwezi kuelewa, sielewi hilo, kuna watu wengi ambao hawawezi kuelewa kwa nini haitwi...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesema haelewi ni kwa nini, Karim Benzema, haichezei timu ya Taifa ya Ufaransa baada ya straika huyo kufunga mabao mawili na kutoa pasi moja ya mwisho wakati Real Madrid ikishinda 3-1 dhidi ya Celta Vigo.

**Mchezo huo uliopigwa juzi, Jumamosi ulikuwa wa mwisho kwa LaLiga kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa wiki hii.**

Benzema alifunga bao la kwanza dakika ya 20 pale Balaidos, na jingine la pili dakika 10 baadaye yote pasi akipata kutoka kwa Toni Kroos na kuiondoa Barcelona kwenye nafasi ya pili na kupunguza gepu la pointi na vinara Atletico Madrid kuwa wa tatu.

Mabao hayo mawili yanamaanisha kwamba, Benzema ambaye hajaitwa kwenye kikosi cha Ufaransa na kocha, Didier Deschamps tangu mwaka 2015 - ana mabao 17 ya ligi msimu huu, na amefunga mabao nane katika mechi sita zilizopita kwenye mashindano yote.

"Huwezi kuelewa, sielewi hilo, kuna watu wengi ambao hawawezi kuelewa hilo," alisema Zidane, wakati alipoulizwa kwa nini Deschamps hataki kumwita Benzema.

"Kwa upande wangu mimi kama kocha wa Real Madrid, ni bora kabaki na sisi, kwa uhakika kabisa.

"Kile alichokifanya leo (juzi) na wachezaji wenzake ni cha kuvutia. Anajituma sana na anataka zaidi."

Benzema kutemwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa mwaka 2015 kulikotana na tuhuma zake na kuhusika kuuvujisha mkanda wa ngono wa mchezaji mwenzake wa zamani wa timu ya taifa, Mathieu Valbuena. Awali, Shirikisho la Soka la Ufaransa liliamua kumweka pembeni Benzema na baadaye Deschamps akamwondoa kwenye kikosi cha Euro 2016.

## ZISIKUPITE

### SHAW KUPEWA MKATABA

MANCHESTER United inajiandaa kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mlinzi wake wa kushoto, Luke Shaw, huku beki huyo mwenye umri wa miaka 25 akifurahia kiwango bora zaidi kwa sasa. ***(Mirror)***

### GARAY KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL imefikia pazuri kwenye mazungumzo na mlinzi wa zamani wa Real Madrid na Argentina, Ezequiel Garay mwenye umri wa miaka 34, ambaye atakuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu. ***(El Gol Digital, via Express)***

### SANCHEZ ATAKIWA SEVILLA

SEVILLA inataka kumsajili mlinzi wa kati wa Tottenham na Colombia, Davinson Sanchez mwenye umri wa miaka 24, ili kuziba pengo la Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, ambaye anatakiwa na Manchester United na Arsenal. ***(Team Talk)***

### BRANDT KUUZWA ARSENAL

KLABU ya Borussia Dortmund ipo tayari kumuuza kiungo wake mwenye umri wa miaka 24, Julian Brandt kwa pauni milioni 21.5, ambaye awali alikuwa akihusishwa na Arsenal. ***(Bild, via Team Talk)***

### NETO AWANIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inataka kumsajili winga wa Wolves, Pedro Neto mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ureno, ambaye ada yake inatajwa kuwa pauni milioni 50. ***(Sun)***

### RUDIGER NA MKATABA CHELSEA

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, ameiambia klabu yake hana mpango wa kuingia kwenye mazungumzo ya mkataba mpya hadi baada ya michuano ya Euro 2020. ***(Athletic via Mail)***

### VAZQUEZ AWINDWA LONDON

TOTTENHAM Hotspur na Arsenal zinawania kumsajili winga wa Real Madrid, Lucas Vazquez mwenye umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

### ALABA KUTUA REAL MADRID

MLINZI wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, anajipanga kujiunga na Real Madrid baada ya miamba hao wa Hispania kumpa ofa ya mshahara wa pauni 165,000 kwa wiki na bonasi ya pauni milioni 17. ***(Sun)***

### CAVANI KUBAKISHWA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema watafanya kila kitu kuhakikisha wanambakiza straika, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, hapo Old Trafford msimu ujao. ***(Mirror)***

### GUENDOUZI KURUDI ARSENAL

KIUNGO Matteo Guendouzi atarudi Arsenal kipindi cha majira ya joto kutoka Hertha Berlin anakocheza kwa mkopo, baada ya miamba hao wa Ujerumani kutokuwa na mpango wa kumsajili moja kwa moja nyota huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Bild, via Mirror)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA, NAMUNGO ZAIAMSHA KMC FC USHINDANI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa KMC, Habib Kondo, amesema kuwa lengo la KMC kwa sasa ni kurejea kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao kama ilivyofanya 2019 ilipocheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Akizungumza jijini Dar es Salaam kuhusu malengo ya msimu huu, Kondo alisema kwa hali ambayo wamefikia, wanatafuta nafasi tu ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao, kwani kuna uwezekano huo kutokana na klabu za Simba na Namungo kufanya vema kwenye mechi za kimataifa.

"Mwanzoni kila timu inakuwa na lengo la kutwaa ubingwa. Lakini ligi inapozidi kwenda kila timu inakuwa inajua nafasi yake iko wapi. Hata sisi ni hivyo hivyo. Kwa sasa akili yetu ni kumaliza kwenye nafasi nne za juu ambazo zinawezekana kabisa zitakuwa na faida msimu huu, kwa sababu huenda tukapata nafasi nne kutokana na mwenendo wa wawakilishi wetu wa sasa, nafasi zinaweza kuongezeka," alisema.

KMC kwa sasa inakamata nafasi ya tano kwa pointi 35 ilizonazo baada ya kucheza mechi 24. Timu hiyo ilicheza kwa mara ya kwanza michuano ya kimataifa mwaka 2019 baada ya kumaliza Ligi Kuu msimu wa 2018/19 ikikamata nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu.

Ilipata nafasi hiyo baada ya Simba kufanya vema kwenye mechi za kimataifa kwa kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, hivyo kuifanya timu hiyo kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Kilichofanyika ni kwamba Simba na Yanga zilicheza Ligi ya Mabingwa, Azam iliyotakiwa kucheza Kombe la Shirikisho kwa kushika nafasi ya tatu kwenye ligi, yenyewe ilitwaa Kombe la FA, hivyo kuwa na sifa ya kucheza michuano hiyo, na kutoa nafasi kwa KMC, kuchukua nafasi ya mshindi wa tatu.

KWAHERI...



Kwaya ya Kijitonyama, Dar es Salaam wakiimba wimbo wa maombolezo wakati wa kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Dansi waachia 'Kalale Pema Peponi Magufuli'*

**Na Adam Fungamwango**

WANAMUZIKI wa dansi Tanzania, wameingia studio na kurekodi wimbo wa kumlilia aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli aliyefariki dunia, Machi 17, Dar es Salaam.

Wanamuziki hao wakiongozwa na mkongwe Maximillian Bushoke, mwanamuziki wa zamani wa DDC Mlimani Park, wametoa wimbo unaoitwa 'Kalale Pema Peponi Dk. Magufuli', ambao umerekodiwa kwenye studio ya Tona de Tona Kinondoni, Dar es Salaam, na upo kwa njia ya 'audio' na video na tayari umeshaanza kusambazwa kwenye vituo mbalimbali vya redio na televisheni.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa Chama cha Muziki wa Dansi Nchini (CHAMUDATA), Hassan Msumari, alisema wameamua kukusanyika wanamuziki wa Tanzania na kutoa wimbo huo ili kuonyeshwa jinsi walivyogushwa na msiba huo.

Alisema mbali na kwamba wanamlilia Magufuli kama Rais wa Tanzania, lakini pia ni kama mwanamuziki mwenzao kutokana na kuwa na kipaji kikubwa cha kupiga ala ya tumba kwenye mikutano yoyote anayokwenda na kukuta kuna muziki wa dansi.

"Ni Rais, ni mwanamuziki mwenzetu. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kupiga chombo cha muziki wa dansi aina ya tumba. Na siyo kama alikuwa anapiga tu. Anajua na anapiga kwa kufuata mirindimo ya muziki kwa ustadi wa hali ya juu.

"Kwenye mikutano yake, tangu akiwa waziri hadi kuwa rais, alikuwa anapenda muziki wa dansi uwapo. Na akifika akimaliza hotuba yake anakuja kwenye chombo chake anapiga kwenye bendi yoyote ambayo ipo hapo, wakati mwingine hadi wimbo utakapokwisha. Kusema kweli tumeumia," alisema Msumari.

Aliwataja wanamuziki ambao wameingia studio mbali na Bushoke, ni Abdallah Hemba, Mackey Fanta, Samat Rajabu, Ramadhani Mhoja, Matei Joseph, Jado FFU, Abdallah Tungwa, Liva Sultan, Jimy Manzaka, Mule FBI, Trsia Masela, Mwezi Mpya, Achuda Bikoo, Shomari Ally, Mjusi Shemboza, Kassim Mafanya, Yusuph Subwa na Kanku Kelly.

## Nyoso, beki Prisons vinara kadi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BEKI mkongwe nchini Juma Nyoso ambaye anaichezea Ruvu Shooting na beki mwingine mkongwe wa Tanzania Prisons, Nurdin Chona, wanaongoza kwa kuwa na kadi nyingi za njano kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Kwa mujibu wa rekodi na takwimu za Ligi Kuu, mabeki hao wana kadi saba za njano kila mmoja na kuwa vinara wa kadi nyingi za njano kwenye ligi ambayo kwa sasa imesimama kupisha maandalizi na mechi za timu ya Taifa, Taifa Stars inayojiandaa na mechi za AFCON.

Wakati mabeki hao wakiwa vinara, kiungo mkabaji wa JKT Tanzania, Kelvin Nashon anafuatia, akishika nafasi ya pili kwa kuwa na kadi nyingi za njano.

Nashon, anayesifika kwa kucheza rafu nyingi kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu, ameonyeshwa kadi za njano mara sita. Wachezaji ambao mpaka sasa wana kadi tano za njano kwenye ligi ni Baraka Mtui wa Gwambina FC, Wema Sadoki na Ihefu na Emmanuel Mvuyekule wa KMC.

Wengine ni Lamine Moro wa Yanga, Andrew Vicent wa KMC na Abdulswamad Kassim wa Kagera Sugar ambao wote wameonyeshwa kadi tano za njano mpaka sasa wakiungana na kipa wa Prisons, Jeremiah Kisubi.

## Kipanga yabadili malengo Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kipanga imesema itaendelea kujifua kwa bidii ili lengo lake la kubaki Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao, litimie baada ya kushindwa kujipa matumaini ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Kipanga imeanza vibaya katika mzunguko wa pili kutokana na kufungwa michezo minne mfululizo kati ya mitano iliyocheza.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha wa timu hiyo, Rashid Lato, alisema tayari amekaa na wachezaji wake na kuwapa somo la saikolojia ili kuondoa hofu ya mchezo husussan katika kipindi hiki cha kuelekea kumaliza ligi hiyo.

Alisema wachezaji wake katika mzunguko wa kwanza walikuwa wanafanya vizuri hadi kufikia hatua ya kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo lakini mzunguko huu wa lala salama wamekuMbwa na hofu kubwa ya mchezo hali inayowasababishia kupoteza mechi.

# Michezo

Jumatatu Machi 22, 2021

Nipashe




Kauli 5 za Dk. Magufuli za kukumbukwa michezoni UKURASA 14

NI MAJONZI...



Baadhi ya viongozi na wachezaji wa Yanga, wakiwa katika foleni ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mfaransa wa Yanga mapema kwa Mkapa

## ●●● Sasa kimeeleweka, kuishuhudia ikiivaa KMC FC Ligi Kuu Bara baada ya....

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga atatangazwa rasmi mwishoni mwa mwezi huu ama mapema Aprili wakati ligi hiyo itakaporejea rasmi wakati huu ikiwa mapumzikoni kupisha kalenda ya kimataifa, kwa mujibu wa uongozi wa klabu hiyo.

**Kocha huyo ambaye ni raia wa Ufaransa, atakuwa jukwaani Uwanja wa Benjamin Mkapa kumshuhudia Juma Mwambusi akiiongoza Yanga kuikaribisha KMC FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara Aprili 7, mwaka huu.**

Yanga ilikuwa katika mchakato wa kumpata kocha mkuu atakayerithi mikoba ya Mrundi Cedric Kaze, ambaye alitimuliwa Machi 7, mwaka huu, baada ya uongozi kukerwa na mwenendo mbaya wa matokeo ya timu kwenye mechi za Ligi Kuu Bara.

Yanga kwa sasa ipo chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Mwambusi, aliyekabidhiwa kukiongoza kikosi hicho hadi mwishoni mwa msimu ndipo Kocha Mkuu achukue nafasi yake.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kila kitu kipo tayari na kilichobaki ni kumtambulisha kocha mkuu mwishoni mwa mwezi huu ama mwanzoni mwa Aprili.

Huku akikataa kumtaja jina, Bumbuli alisema kocha huyo ni raia wa Ufaransa ambaye amekidhi vigezo walivyokuwa wanavitaka na si kwamba wamefanya hivyo kutokana na watani zao, Simba kunolewa na Mfaransa Didier Gomes da Rosa.

"Mwishoni mwa mwezi huu ama mwanzoni mwa mwezi ujao tutamtangaza rasmi kocha mkuu, subirini mtamjua. Ni raia wa Ufaransa, tumemchukua kutokana na kukidhi vigezo tulivyokuwa tunavitaka na si kwa sababu ya watani zetu kunolewa na Mfaransa," alisema.

Kuhusu Wafaransa wawili wanahusishwa na klabu hiyo Hubert Velud anayeinoa timu ya Taifa ya Sudan na Sebastien Migne, aliyewahi kuinoa timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars, Bumbuli alisema muda ukifika wa kumtangaza atajulikana.

Licha ya Bumbuli kukataa kutaja jina moja kati ya hayo mawili, chanzo cha uhakika kutoka ndani ya klabu hiyo, kimeliambia Nipashe kuwa ni Velud ndiye atakayeinoa timu hiyo ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 50 baada ya mechi 23.

Hata hivyo, Yanga ambayo imepania kutwaa ubingwa msimu huu, ina kazi kubwa ya kutimiza malengo hayo kutokana na watani zao, Simba waliopo nafasi ya pili wakiwa na pointi 46 zilizotokana na kushuka dimbani mara 20, kupania kutetea taji hilo kwa mara ya nne mfululizo.

Ligi hiyo kwa sasa ipo mapumzikoni kupisha maandalizi ya mechi za kimataifa kwa Taifa Stars ambayo itacheza dhidi ya Equatoria Guinea na Libya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021.

# Simba ikipasua CAF, Miquissone kutoboa

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA wa Klabu ya Simba, Luis Miquissone, amejiweka katika nafasi nzuri ya kuwamo katika kikosi bora cha michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu wa 2020/21, kutokana na ubora anaoendelea kuonyesha wakati huu timu yao ikiwa hatua ya makundi.

Tayari Miquissone ameingia mara mbili katika kikosi bora cha CAF cha Ligi ya Mabingwa huku pia akichaguliwa kuwa mchezaji bora wa wiki wa michuano hiyo, ambayo timu yake ya Simba inaongoza Kundi A ikiwa na pointi 10 kileleni mbele ya mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri yenye alama saba, AS Vita ya DR Congo pointi nne na Al-Merrikh ya Sudan inayoburuza mkia kwa pointi yake moja.

Miquissone alichaguliwa kuingia katika kikosi bora cha CAF katika raundi ya pili ya michuano hiyo wakati akiifungia Simba bao pekee lililoipa ushindi 1-0 dhidi ya Al Ahly kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambapo pia alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi na wa wiki wa michuano hiyo.

Katika orodha hiyo, alikuwapo pia beki wa Simba, Joash Onyango aliyeingia katika kikosi hicho cha CAF, lakini Miquissone alizidi kuonyesha ubora katika mchezo uliofuata dhidi ya Al-Merrikh na kutangazwa tena katika kikosi cha wiki wakati huu akitangazwa pamoja na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Kwenye mechi hiyo ambayo Simba ilishinda 3-0 katika Uwanja wa Mkapa, Tshabalala alifunga bao moja huku Miquissone akifunga na kutoa pasi ya mwisho, jambo ambalo kama akiendelea na ubora huo, hakuna kitakachomzuia kuingia katika kikosi bora cha CAF cha msimu huu wa Ligi ya Mabingwa Afrika endapo Simba itasonga mbele hadi hatua ya fainali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002